

IMETUPASA KUTIMIZA HAKI YOTE

 Daima ni majaliwa kuja kwenye nyumba ya Bwana. Kamwe, maishani mwangu, sijaona wakati mmoja nilijutia kuja kwenye nyumba Yake. Ni ninii... Lakini ninadhani asubuhi ya leo ndio wakati mgumu kuliko zote nilizopata kuja. Naam, hiyo ni kweli. Kwa hiyo, mambo hutendeka maishani, tunajua hilo, ambayo hatuna budi kuyakabili. Nasi hatuna budi kukumbuka hilo, kwamba yanawajilia wote.

² Nasi tunashukuru sana asubuhi ya leo, ninashukuru, na ninajua ndugu zangu na dada wanamshukuru Mungu sana, kujua ya kwamba mama yetu ameokoka.

³ Naye ni mzee, nasi tumekuwa tukilitarajia hili kwa muda fulani, kwa kuwa yeye ni mama wa wengi, naye ameyavunja maisha yake. Katika siku za mama yangu, hawakuwa na vitu walivyo navyo leo hii, kuwahudumia akina mama walipowazaa watoto wao. Huenda ikawa, labda, mama angemzaa mmoja wa hao watoto asubuhi hiyo, kisha aamke na kufua nguo alasiri hiyo. Na kwa hiyo sasa wanalala hospitalini siku kadhaa, pamoja na kila namna ya matibabu, yaliyopo. Tunashukuru kwa ajili ya vitu kama hivyo vinavyoweza kuwasaidia hawa, mama hawa na wote.

⁴ Yeye yuko karibu sana, sana na kufa sasa. Nami... [Ndugu Branham analia—Mh.] Ni ninii—jambo gumu tu asubuhi ya leo, lakini hata hivyo ni—niliahidi kuwa hapa. Nami ninaninii...

⁵ Sasa, siwezi kusema ya kwamba mama yangu anatuacha. Mara nyingi nimesema jambo hili. Na wengi ni mashahidi, kuhusu maono. Nilisema, “Kama mama yangu mwenyewe alikuwa amelala, akifa, na kuuangalia uso wangu na kusema, ‘Billy, i—itakuwaje kwangu?’” Nilisema, “Isipokuwa Mungu aniambie, nisingejua. Ni—nisingeweza kusema.” Na jambo lilo hilo limetimia. Kama mama anatuacha, Yeye amelifanya siri kwangu.

Kabla baba yangu hajafa, niliona ono lake akituacha.

⁶ Nilipokuwa ningali mwenye dhambi, nilimwona ndugu yangu, wa kwanza, alikuwa anatuacha.

⁷ Howard. Niliwaambia ninyi nyote, miaka miwili ama mitatu kabla hajatuacha, kuhusu kuondoka kwake.

⁸ Lakini, mama, Yeye hajaniambia neno. Na endapo anatuacha, ni jambo ambalo silijui. Ingawa, tulikuwa... Dakitari amesema hakuelewa jinsi alivyoishi akamaliza Jumapili iliyopita. Naye ni mahututi sana. Lakini, hata hivyo, nilipokuwa...

⁹ Yapata mwezi mmoja uliopita, kama nilivyomfanyia Bibi Broy; sikuzote mimi hupenda kuwajulia watu hali, kujua ya kwamba wamekaribia mwisho, kwamba nione hali yao. Inatupasa kuwa na hakika ya hili. Hatutaki tu kusema, “Vema, labda ni vema.” Tunataka kuwa na hakika kwamba ni kweli.

¹⁰ Nilikuwa na mazungumzo mazuri marefu asubuhi moja na mama. Akasema, “Billy, ni—nimeishi kadiri ninavyopaswa kuishi.” Akasema, “Sina lingine la kuishia.” Akasema, “Sina budi kuwaacha.” Kisha kasema, “Ni afadhali niende, kuwa pamoja na baba na baadhi ya hao watoto wengine walioko Kule. Mimi huwaona ninyi nyote, mara nyingi.”

¹¹ Ndipo wakati alipokuwa akiwekwa kwenye gari la kuchukulia wagonjwa, kumpeleka hospitalini, akapewe glukosi, maana asingeweza kula chochote. Iliwabidi kumpa glukosi kupitia kwenye mishipa yake. Ndipo nikamwambia, wakati tukimwingiza kwenye gari la kuchukulia wagonjwa, nikasema, “Sasa, mama, kila kitu ni shwari.”

Akasema, “Ninatamani kuwaacha.”

¹² Nami nikasema, “Mama, kama ulikuwa ukiniachia hazina duniani, ya dola milioni mia moja, kwa ajili yetu sisi watoto, ama ulikuwa ukituachia nyumba ambayo ingetoka mji mmoja hadi mwingine, kamwe isingelinganishwa na ushuhuda huu unaotuachia, ‘Niko tayari kuwaacha.’” Ni hazina ambayo fedha haziwezi kununua, kujua hilo.

¹³ Kwa hiyo basi, kwa jambo hilo, ninasimama kwa ujasiri, nikiamini mambo haya ambayo nimehubiri. Hili linamfaa mama yangu, linawafaa mama wa watu wengine, linatufaa sisi sote. Nisingeweza kusema, “Mungu, usimchukue.” Kwa sababu, ninajua ya kwamba mara nafsi yake ya kibinadamu itakapouacha mwili huu, ana mwingine unaongoja. Naye atakuwa msichana tena, katika dakika chache tu baada ya kuondoka hapa.

¹⁴ Je! mlipata kuona mtoto mchanga wakati akizaliwa, misuli yake midogo ikishtuka-shtuka na kucheza? Lakini anapoingia duniani, yeye hupokea roho fulani, ndipo anakuwa nafsi iliyo hai. Na mara hiyo nafsi ikirudi kutoka kwenye mwili huo mdogo, kuna mwingine unaongojea. Mnaona? Kwa sababu, kwanza, Mungu huumba nafsi na roho, inaingia tu miilini. Na, na tunapoondoka hapa, tunabadilisha tu makao yetu na kuingia kwenye mengine. “Kwa maana maskani hii iliyo ya dunia ikiharibika, tunayo nyingine inayongoja.” Kwa hiyo, hiyo ndiyo faraja yetu.

Sasa na tuombe.

¹⁵ Baba yetu wa Mbinguni, Mwenye Utukufu, tungefanya nini katika nyakati hizi zenye haja nyingi mno, kama isingalikuwa ni kwa ajili Yako? Lakini tumaini letu halijajengwa juu ya kingine chochote pungufu ya Damu ya Yesu na haki Yake! Nasi tuna

furaha sana kujua ya kwamba kuna Nchi ng'ambo ya mto. Ya kwamba utakapomaliza nasi katika dunia hii, ya kwamba tunabadilisha tu makao yetu, kwenda kwenye ile Nchi yenye utukufu, huko ng'ambo, ambako hakuna maradhi wala huzuni, mauti wala utengano. Daima tutakuwa pamoja na Wewe na pamoja na wapendwa wetu. Kwa hiyo, tunakushukuru kwa ajili ya tumaini hili zuri mno lililo mioyoni mwetu leo hii.

¹⁶ Na ilionekana, Bwana, ni vigumu kwangu asubuhi ya leo kushuka huku; sio kukutumikia, bali nikijua ya kwamba nina wasiwasi na nashangaa jinsi nitakavyoweza kuuendea Ujumbe huu asubuhi ya leo kwa ajili ya kanisa, ambao ninajisikia kwamba umeuweka moyoni mwangu. Jinsi adui amenizungusha-zungusha nao! Lakini nimefikia umbali huu, mimbarani, katika Jina Lako. Nami ninajikabidhi, pamoja na Ujumbe na vyote, mikononi Mwako, na najua kwamba Wewe unaweza hata na zaidi kuuingiza kwenye kila moyo, na kutupatia kila kitu tunachohitaji. Tunayakabidhi yote Kwako sasa, na sisi wenyewe, kama utumishi Wako; kwa kuwa midomo yangu ndiyo mnenaji Wako, na masikio kama kituo Chako cha kusikizia. Tubariki, Bwana.

¹⁷ Na wajalie mama wengine, akina baba, na wale watakaokuwako katika siku zijazo, kama ulimwengu utasimama, jalia wajiandae na wajue, pia, ya kwamba hawana budi kushuka siku moja kwenye saa hii ambayo mama amefikia. Naomba, Mungu, ya kwamba watafanya maandalizi yao leo hii. Kwa kuwa hakuna jambo jingine moja ulimwenguni linalojalisha. Hakuna fedha zinazoweza kununua, hakuna kupendwa na watu kunakoweza kudumisha; hamna kitu kinachoweza kusaidia ila Mungu, na Mungu pekee. Nasi tunashikilia kwenye mkono Wake usiabadilika, tukijua ya kwamba Yeye amesema, "Hatua za mwenye haki zinaimarishwa na Bwana." Kwa hiyo mateso haya madogo tuliyo nayo sasa, katika maisha ya sasa, hayatakuwa na maana sana. Kama vile mshairi amelielezea, "Masumbuko ya safarini yataonekana kama si kitu, tutakapofika mwisho wa safari."

¹⁸ Tusaidie, Bwana, tukaze mwendo kuelekea kwenye mede ya wito mkuu, tukijua ya kwamba siku moja, huko ng'ambo kuu ya hapa, tutakutana mahali pema hivi karibuni. Yabariki Maneno Yako sasa. Wabariki watumishi Wako. Kila mtoto wa Mungu aliye hapa ndani, jalia mioyo yao ipashwe moto na kuchochewa asubuhi ya leo. Na, Baba, ninahitaji baadhi yake, mimi mwenyewe. Ninaomba ya kwamba utayajalia, mambo haya yote, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

¹⁹ Sasa niliona ya kwamba hapa tuna lundo la lesa. Nami ninaninii . . . Tutazifikia katika muda mfupi.

²⁰ Nimetoka kwenye safari ambako nimekuwa kwenye safari ya kuwinda, pamoja na mtu fulani huko juu karibu na Alaska.

Mwajua, msimu huu kwa namna fulani ni msimu ninaoutenga, msimu wa kupukutika majani mwakani, kujijenga mwenyewe tena, nikijiandaa kwa ajili ya misimu iliyo mbele kwa ajili ya ibada.

²¹ Sina nguvu sana, vema, ningesema, kwenye neva zangu. Nina mfumo m—mbaya sana wa neva. Nami ninatambua ya kwamba inahitaji mfumo wa namna hiyo kuifanya huduma ambayo Bwana amenipa. Huwezi kuwa na mambo yote yakienda vizuri sana, duniani. Kimwili, ninashukuru sana kwa ajili ya mwili wenye nguvu. Lakini mfumo wangu wa neva, kwa sababu unatenda kazi moja kwa moja kati ya mambo ya kawaida na ya kimbinguni, nayo yanakuraru vipande-vipande. Wala kamwe sijajaribu kuketi chini na kulielezea hilo kwa makusanyiko yangu, kwa maana wasingeelewa, kwa kuwa sielewi, mimi mwenyewe. Lakini hata kwa madaktari, walinichunguza na kuweka jaribio hilo la neva; wakasema kamwe hawajapata kuona kitu kama hicho, mnaona, jinsi itakavyotoka mahali pamoja, moja kwa moja mpaka hapo pengine. Sielewi utafiti wao wa sayansi na, ama kile wamefanya, njia zao za kufanya mambo. Lakini ninajua ya kwamba kuna jambo lililonipata siku moja, hapo Kristo aliponishika, nilibadilishwa.

²² Nami ningetaka tu kusema jambo hili, huenda likanihuisha. Inaonekana kana kwamba lingekuwa ni jambo lisilo kawaida kabisa, kulizungumzia, asubuhi ya leo. Lakini ninii tu, kabla ya kuingilia Ujumbe wangu, ili kujituliza kwa namna fulani, ningetaka kusema hilo. Nilipotangaza kwamba nitakuwa hapa, sikuja ya kwamba mama angekuwa mgonjwa.

²³ Na pia nilitangaza ibada ya usiku huu. Mungu akipenda, tutaifanya. Nitakuwa hapa usiku wa leo, kuhubiri, kama hilo ni sawa kwa mchungaji. [Ndugu Neville anasema, “Naam, bwana!”—Mh.] Nami ninataka kuzungumza juu ya, *Mfariji Amekuja*, usiku wa leo. Na halafu hiyo ni ibada ya usiku wa leo. Nasi tuna ibada ya ushirika hapa usiku wa leo. Na watu wote wamealikwa kwa moyo mkunjufu waje wa—wale ushirika huu pamoja nasi usiku wa leo, na kwa ajili ya Ujumbe.

²⁴ Ilikuwa ni majira yaliyopita ya kuchipusha nilipokuwa huko Alaska, ama huko juu karibu na Alaska, katika British Columbia, kuninii...kwa ajili ya ibada, ambapo Bwana alitupatia wakati wa ajabu sana. Nami daima ni—nimependa kuwa porini.

²⁵ Mnaweza kunisikia vizuri huko nyuma? Mnaweza...Kama mnaweza, inueni mikono yenu, huko nyuma kabisa.

²⁶ Daima nimependa kuwa porini. Kama vile mtu yeyote anayeijua familia yetu, anajua hivyo kule. Mama yangu, anayekufa huko nje sasa, mama yake alikuwa ni Mhindi. Na wongofu wangu haukubadilisha hilo, nami...kupenda kwangu kuwa porini, nami nina furaha, kwa maana ndipo mahali

ninapomwona Mungu. Siendi sana sana kuwinda wanyama, ni—ni kuwa peke yangu pamoja na Mungu. Nami huwinda peke yangu.

²⁷ Na wakati nikiwa huko nje, nilikutana na viongozi wazuri mno. Hao ndio wale jamaa, huko Kanada na mahali mbalimbali, kabla hujaweza kuingia nyikani, shirika la wanyama linakuteulia kiongozi. Na huyo kiongozi hana budi kuwa pamoja na wewe.

²⁸ Basi nilikutana na ndugu mzuri sana Mkristo, kijana, mpentekoste, aliyekuwa kiongozi aliyesifika sana Kanada. Mke wake alikuwa mwanamke mzuri sana, aliyeokoka. Naye ana umri upatao miaka arobaini, na alikuwa na watoto watano wadogo, wavulana wadogo, kutoka umri wa miaka kumi na minane hata kwenye miaka miwili. Naye alikuwa amepewa sehemu kubwa ya maili mia tano ya Barabara ya Alcan, kuwa eneo lake la kuongozea.

²⁹ Kuna baadhi ya Wahindi huko nyuma, ambao hawakutaka kuhama, nao walikuwa wenye kiburi sana, hata wakaweka ubao, “Mkija huku, kutatokea umwagikaji wa damu.” Lakini, hata hivyo, tulipanda farasi tukapita hapo, kisha tukarudi, kwa kuwa nilitaka kuzungumza na Wahindi hao. Hata hivyo, nchi hii ilikuwa ni yao kabla haijakuwa yetu, mwajua. Nami nilikuwa na wakati mzuri nao, majira yaliyopita ya kuchipusha, nikiwaambia kuhusu Bwana Yesu.

³⁰ Ndipo mzee mmoja, baba mkongwe wa kabila hilo, alikuwa karibu na umri wa miaka mia moja. Alikuwa na ninii yake... Ningeweza kuona ni kwa nini hakutaka kuhama. Wao huwazika wafu wao katika gogo, kisha wanalitundika gogo hilo juu kwenye mti. Walikuwa na watoto wadogo wawili wamezikwa pale. Hakika, hakutaka kuhama. Ninaweza kuona ni kwa nini yeye hakutaka kuhama. Nayo hifadhi, se—serikali ya Kanada, Utawala wa Kanada ulisema, “Wakiwa na kiburi, watawaondosha tu huko na kuwahamisha.” Mbona, usingewataka wafanye hivyo; wototo wao wachanga wemening’inia pale mitini.

³¹ Na kwa hiyo, hata hivyo, mito ilishuka na kutukatilia mbali na tusingeweza kurudi kwenye maeneo tuliyokuwa tukienda kuwindia dubu wa kijivu. Huyu Bw. Southwick, ni Southwick, alikuwa ndiye kiongozi. Naye... Nami nilikuwa pamoja na maskini mhudumu mdogo, Eddie Byskal. Na kwa hiyo mvulana wake... Bw. Southwick alikuwa—alikuwa na ndugu mdogo, yapata, kati ya umri wa miaka ishirini na mitano na thelathini, alikuwa hawezi kabisa kwa kifafa.

³² Bw. Southwick ndiyo kwanza tu awe Mkristo, yapata mwaka mmoja uliopita. Hapo awali ni kaoboi, na kidogo wao wanaparuza, mwajua, katika maisha yao. Na, lakini ndiyo kwanza tu awe Mkristo, naye alikuwa akiamini. Ndipo akasema,

“Nilikisoma kitabu chako, Ndugu Branham.” Naye akaendelea kuligusia kidogo, akidokezea, kuhusu ndugu yake mwenye kifafa. Akasema, “Loo, laiti ningalimleta ndugu yangu kwako!” Vema, unajua jinsi inavyokufanya ujisikie, huna la kufanya, huwezi kufanya kitu, nawe unashangaa tu jinsi ambavyo yote yangeweza kutukia.

³³ Halafu huko Kanada, kwa kawaida watu ambao...Ninyi watu mnaofanya safari, mnajua, katika kuwadhibiti farasi. Nami ninawapenda farasi na wanyama. Kwa kawaida wao hufunga hatamu kwenye mkia, na kuwafanya watembee katika mstari, mwambatano. Lakini kule usingeweza kufanya hivyo, kwa sababu ya mwambatope; ukimpoteza farasi mmoja, huenda ukaupoteza mlolongo wote. Kwa hiyo inatubidi tu kuwaachilia waende, na kuwasukumiza kwenye kinjia.

³⁴ Nami nilikuwa huko nyuma kabisa, juu ya farasi mchanga, nikijaribu kuwakusanya waliopotea na kuwarudisha. Ndipo Roho Mtakatifu, katika neema Yake, akashuka. Nikamchochea farasi wangu, nikampanda nikaupita mstari huo, mpaka mahali Bw. Southwick alipokuwa akiongozea, huko mbele, kupitia kichakani. Ndipo nikasema, “Bud?”

Akasema, “Naam, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Utaliadini Neno langu?”

Akasema, “Pamoja na chochote utakachosema.”

³⁵ Ndipo nikasema, “Nina BWANA ASEMA HIVI kwa ajili yako.” Nikasema, “Nenda ukamchukue ndugu yako kutoka Fort Saint John,” ambayo iko umbali wa maili mia saba ama mia nane, “ukamlete kwenye barabara kuu hapa.” Naye aliishi kwenye kibanda cha kale akiwa na stovu ya salamanda, alikuwa na watoto wake kule. Ndipo nikasema, “Mara ya kwanza atakaposhikwa na kifafa, nyakua shati lake kutoka mgongoni mwake. Nitakupa cha kufanya. Litupe motoni, na useme, ‘Hili nalitenda katika Jina la Yesu Kristo.’”

Akasema, “Nitafanya hivyo.”

³⁶ Kwa hiyo akaenda, akamtuma mtu na kumpata ndugu yake, akamleta kule. Basi asubuhi hiyo ilibidi atoke aende kufuatilia pamoja na mtu wa uhifadhi. Naye ndugu yake kwa kawaida hushikwa na kifafa hicho mara mbili ama tatu, kwa siku, naye amekuwa nacho tangu alipokuwa mvulana mdogo. Naye mke wake alikuwa anamwogopa sana, huyo, wakati alipokuwa na hicho kifafa, kwa kuwa alikuwa mkali; jamaa mdogo, mwenye nguvu sana.

³⁷ Ndipo akashikwa na kifafa, baada ya Bud kuondoka. Badala ya kuruka atokee dirishani, kama alivyofanya kwa kawaida, akiwaondosha watoto wake, alimrukia tu moja kwa moja, akalinyakua shati lake; maskini mwanamke mdogo, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akalinyakua shati lake na kulitupa motoni,

na kusema, “Nafanya hili kwa Jina la Yesu Kristo.” Kamwe hajapata kushikwa na kifafa tangu wakati huo. Hayo yalikuwa ni majira ya kuchipusha yaliyopita.

³⁸ Mara nyingi, ninajua imekuwa ni vigumu kidogo. Watu ambao wasingefahamu, wanasema, “Ndugu Branham, ni kwa nini wewe hufanya safari ya kuwinda?” Mnaona, kamwe hawaelewi. Hakuna haja ya kujaribu kulielezea, mnaona. Unawashika watu kule ambao kamwe wasingeweza kushikwa.

³⁹ Yapata miezi miwili iliyopita, ama si muda mrefu hivyo, niliamshwa asubuhi moja. Ninaamini, sina hakika, nililisimulia kwa karibu kanisa zima. Wapo wengi hapa wamenisikia nikilisimulia hili kabla halijatukia. Na kwenye ono niliona, kwamba nilikuwa nimemwona mnyama mkubwa sana, alionekana kama kulungu. Naye alikuwa na pembe kubwa, ndefu. Na alikuwa... Ilinibidi kuzunguka upande mmoja, mwambatope, namna *hii*, kumfikia. Naye alikuwa ni mnyama anayejulikana sana. Alikuwa ni mnyama mkubwa wa kumbukumbu. Na kulikuwako na mtu niliyemwona aliyekuwa amevaa shati la kijani kibichi lenye milia. Halafu, barabarani, baada ya kumpata mnyama huyo, nilisikia sa—sauti ikisema kwamba, “Pembe hizo zina urefu wa futi arobaini na mbili.” Huo ni karibu urefu *huu*. Naye alikuwa ni mnyama mkubwa mno. Basi nilipokuwa nikirudi, nilimwona dubu wa rangi ya fedha na kijivu.

⁴⁰ Sasa, huyo ni dubu anayejulikana sana. Wapo wanne katika familia ya dubu wa rangi ya fedha. Mmoja ni wa kijivu, ambaye ndiye anayejulikana sana. Huyo mwingine anaitwa, jina la kienyeji, *kadishi* (?), ambaye ni mweusi, na sikio la duara; wa pili. Wa tatu, ni dubu wa kawaida wa rangi ya fedha, ambaye ni kati ya mweusi na hudhurungi, dubu mkubwa mno. Na huyo mwingine ni Kodiaki, ambaye anapatikana tu katika Kisiwa cha Kodiaki na—na Alaska magharibi; yeye ni jitu kubwa mno, mkubwa sana, dubu aliye mkubwa kuliko wote, bali ni wa rangi ya fedha. Lakini yule wa kijivu ni mweusi, na nyeupe iko kwenye... rangi ya fedha iko kwenye ncha ya manyoya. Ndiye anayejulikana sana, dubu mkorofi sana, mwenye hasira mbaya.

⁴¹ Nilimpiga dubu huyo risasi ya moyoni, nikamwua. Lakini nilikuwa nina tashwishi na hiyo bunduki ndogo niliyokuwa nayo, juu ya kumpata. Nami nilikuwa nimewaambia hao ndugu. Ni wangapi hapa wamenisikia nikisimulia hayo kabla hayajatukia? Inueni mikono yenu. Vema, hakika, karibu wote, mnaona.

⁴² Na kwa hiyo basi Bw. Arganbright aliniita na alinitaka niende Alaska. Vema, badala ya kwenda Alaska, nilijisikia kuongozwa kurudi hapa juu kwenye safari hii, huku juu pamoja na Bud, kwa kuwa nilikuwa nimemwahidi.

⁴³ Nilipofika kule, nilimwambia mke wake na watu wote kule, mambo haya aliyosema. Nikasema, “Lakini, sasa, ni nani kati yenu nyote aliye na shati la kijani kibichi, lenye milia?” Hakuna mtu aliyekuwa nalo. “Vema,” nikasema, “basi haina budi kuwa ni safari nyingine nitakayofanya. Lakini, mahali fulani, Bwana atanipa huyo, kweli kabisa.” Kwa hiyo nikasema, “Nilifikiri huenda ikawa ni safari hii.”

⁴⁴ Vema, tukaendelea, kwenye safari hiyo. Basi siku ya kwanza, wakati tulipofika juu, juu ya mpaka wa msitu, ambapo hamna miti, huko juu ya mito ya barafu, pamoja na farasi wetu. Ndipo kesho yake, tuliwinda wengine, na tukawapata kondoo wengi wenye pembe za theluthi tatu zilizojipindapinda, na kadhalika, bali haikuwa ni sawa kabisa.

⁴⁵ Nawe nena juu ya ushirika, kila mmoja wetu mpentekoste na tulikuwa na Roho Mtakatifu! Tulikuwa na wakati wa ajabu huko juu, na kuziona rangi hizo zikibadilika, na milima hiyo, na huko juu kabisa anakoishi Mungu pekee! Na wakati mzuri jinsi hiyo! Tusingeenda kulala mpaka saa saba usiku, tukimsifu tu Mungu na kuwa na wakati mzuri sana!

⁴⁶ Ndipo kwenye siku ya pili, tulitoka. Na yapata maili sita kurudi, huko nyuma ya mito ya barafu, tuliwaona kondoo dume wakubwa. Nami nikasema, “Vema, tungerudi, na kesho yake kwenye mapambazuko tutakuwa tumeondoka.”

⁴⁷ Kwa hiyo tukaanza kuondoka kesho yake asubuhi, kabla ya mapambazuko; ndipo tukafika, kwenye saa tatu, tulikuwa huko juu kabisa tulikokuwa tumeiona ile mito ya barafu.

⁴⁸ Lakini tulipokuwa tukipanda juu, nilikuwa nimemwona kuro wangu wa kwanza wa mwituni. Kamwe sikuwa nimemwona kama huyo. Nimewaona waliofugwa, huko kwa Lapland, na kadhalika, bali sio katika kuro, ambaye sininii. . . *Kuro* ni jina la kienyeji, ni “kulungu baridi.” Na kwa hiyo kwa kawaida wana pembe za paneli, namna *hii*, moja ikipitia papo hapo mbele ya pua yao, halafu paneli inatokeza mbele; halafu hizo pembe zinapindana, huku zikiwa na paneli nyingine pana hivi.

Bud alikuwa ameniambia, “Labda. . .”

⁴⁹ Nikasema, “La, la. Yeye. . .” Nikasema, “Haikuwa ni kuro, maana hakuwa na pembe za aina hiyo.” Lakini asubuhi hiyo, tukikwea, mbona, nilikuwa nimeona jike la mnyama na mtoto wake. Ndipo tukaenda kando, nami nikamwona, dume mchanga, akikimbia.

⁵⁰ Naye Ndugu Eddie, akitaka kuwalisha Wahindi ambako yeye ni mmishenari. Huyo hapo mtu mzuri, ametoka kwenye nyumba nzuri, na mke kutoka tu kwenye familia nzuri sana. Nayo mikono yao imeliwa *hapa*, na inauma, kwa viroboto, ambako waliishi na Wahindi na kadhalika, huko nje wakijaribu kumleta Kristo kwa Wahindi. Inahitaji neema kufanya hivyo! Wanaishi huko

kwa siagi ya karanga na molasi, na kulala kwenye vibanda hivyo ambamo kunguni, viroboto na kila kitu, wanawauma tu namna hiyo, hata hivyo, wapate kuileta Injili ya Yesu Kristo!

Na kwa hiyo Ndugu Eddie akakizunguka kilima hicho kisiri.

⁵¹ Nami nikaketi tu hapo kwa kicho, kwa saa mbili, nilipoona mlima mkubwa mno wenye kilele cha theluji. Nikawazia, “Bwana Mungu, jalia niishi hapa katika ule Utawala wa Miaka Elfu.” Kuiona mimea manjano itetemekayo chini ya kilima, na vichaka laini vyekundu, na vyote vikipatana na ile milima yenye vilele vya barafu, vikiakisi kwenye maziwa. Kuna kitu fulani tu juu yake, jinsi ambavyo ungeweza kuketi pale na kulia, na kulia na kulia, maana Mungu pekee ndiye angeweza kuzitia rangi hizo. Hakuna kitu kinachoweza kufanya hivyo, mnaona.

⁵² Nami nilikuwa nimeketi pale, ikawa niliwazia, “Vema, nashangaa ni kitu gani kilichompata Ndugu Eddie?”

⁵³ Nikamwendea Bud, naye alikuwa ameketi pale akifurahia jambo hilo, pia, kwa karibu saa mbili. Ndipo tukaamka, nami nikaiona kamera ya sinema ya Eddie imewekwa moja kwa moja kule juu. Juu ya milima ile, hakuna kitu ila kuro, kuvumwani, kuvumwani tu, ni huko juu ya mahali ambapo miti haitamea.

⁵⁴ Nami nikamwona huko chini ya kilima. Alikuwa ameweka vidole vyake juu namna *hii*, alikuwa akimnyemelea dume huyu mchanga wa kuro. Vema, a—alimpiga risasi huyo kuro. Nasi tukamtayarisha tu, kisha tukarudi juu ya kile kilima. Nami nikashuka chini vya kutosha tukachota maji.

⁵⁵ Nami nilikuwa nikiangalia tu kote kwa darubini. Kwa namna fulani, yapata maili mbili kutoka kwangu, huyo hapo mnyama wangu amelala. Nilimwona. Nikasema, “Huyo ndiye. Huyo ndiye.” Nikasema, “Angalieni hapa, angalieni huu mwambatope, inatupasa kuuzunguka.” Ndipo nikasema, “Jambo pekee ni lile ninii la kijani kibichi lenye milia . . .” Ndipo nikaangalia, naye Eddie alikuwa amevaa shati la kijani kibichi lenye milia.

Nikasema, “Eddie, nilifikiri wewe . . .”

⁵⁶ Akasema, “Ndugu Branham, sikuninii. Hapana shaka mke wangu aliliweka mle ndani.” Akasema, “Nilichukua shati safi asubuhi ya leo, lakini sikujua hivyo. Hapana shaka mke wangu aliliweka mle.” Mungu hashindwi jambo moja. Yeye ni mkamilifu tu. Huyo hapo na shati la kijani kibichi lenye milia.

⁵⁷ Huyo kiongozi akasema, “Ndugu Branham, sijui jinsi utakavyomfikia huyo.”

⁵⁸ Nikasema, “Sijali kama yuko umbali wa maili hamsini, yeye ni wangu.” Nikasema, “Yeye ni wangu.” Nasi tukaanza kuuzunguka huo mwambatope, ninii tu, loo, wenye mwinuko mkali *hivi*, kando yake tu.

⁵⁹ Ndipo tukaenda huko, nami nikampata huyo kuro mkubwa. Na—na badala ya kuwa na zile paneli, alikuwa na pembe zilizochongoka; kamwe sijapata kumwona mmoja kama huyo. Mnaona jinsi ilivyo ajabu, jinsi Mungu anavyotenda mambo?

⁶⁰ Kwa hiyo tukawaambia hao wavulana washuke darajani, wawachukue hao farasi na kuichukua nyama, wakakutane nasi huko chini tutakaposhuka. Bila shaka, Ndugu Bud aliangalia kote, kasema, “Ono la Ndugu Branham, kama lilikuwa ni la kweli juu ya ndugu yangu kuponywa, kifafa, yeye atampata mnyama huyo haidhuru yuko wapi.” Kwa hiyo akasema, “Ninyi kutaneni nasi tu, tutampata, tunaelekea huko chini.”

⁶¹ Na kwa hiyo tulipomchuna ngozi; nayo ngozi na pembe, na kila kitu, zingekuwa kama ratili mia moja na ishirini na tano; lakini tu, sio ngozi ya mwili, ngozi ya kichwa pekee. Kwa hiyo basi akasema, “Sasa, Ndugu Branham,” kasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani.” Kasema, “Ingekuwa vigumu kwangu kumchuna ngozi hapa,” sote wawili, mmoja kwenye kila upande. Akasema, “Ati unasema pembe hizi ni ‘futi arobaini na mbili?’”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Zinaonekana kama tisini, kwangu mimi.”

Nikasema, “Ni arobaini na mbili.”

Naye akasema, “Nina utepe wa kupimia kwenye mfuko wangu wa matandiko.”

Nikasema, “Vema, utaona ni kamilifu kabisa.”

⁶² Akasema, “Basi, kulingana na yale uliyoniambia, mahali fulani kati ya hapa na mahali tutakapokutana na hao wavulana, mwenye kuvaa shati hilo la kijani kibichi, utampata dubu mwenye rangi ya fedha na ya kijivu?” Kasema, “Sijapata kumwona mmoja, nami nimeishi kwenye milima hii maishani mwangu mwote.”

Nikasema, “Lakini ni BWANA ASEMA HIVI.”

Kasema, “Unajua mahali alipo?”

⁶³ Nikasema, “La. Lakini yupo mahali fulani kati ya hapa na hao wavulana.” Tungeweza kuona moja kwa moja mpaka walipokuwa, karibu maili tatu, chini kwenye mpaka wa miti. Nikasema, “Tutampata.” Sasa, hilo ni jambo fulani!

⁶⁴ Akasema, “Basi, tutakuwa huko chini katika saa moja na nusu. Nawe unataka kuniambia ya kwamba utampata dubu mkubwa mno wa kifedha, wa kijivu, mahali fulani kati ya hapa na wale wavulana?”

Nikasema, “Hiyo ni kulingana na Neno Lake.”

Akasema, “Yeye yuko.”

⁶⁵ Kwa hiyo tukazibeba zile pembe, juu ya vichwa vyetu, na kuziburura ndipo tukashuka kilimani, hata tukafikia kwenye mito ya barafu. Ndipo tulipofika kwenye mito ya barafu;

kulikuwa na joto sana, ilitubidi kuingia kwenye mito hiyo ya barafu kwa kitambo kidogo, tupate kujipoza. Tukapita mito hiyo ya barafu, tukashuka mpaka tukafika ambapo maji yalikuwa yakitoka chini ya mto wa barafu, na kuingia kwenye ninii... yakaanza kuingia msituni. Tukaketi tu chini, kupumzika.

⁶⁶ Nikageuka, na kuangalia. Nikasema, “Angalia, Bud! Kitu kama ng’ombe, yapata umbali wa maili mbili.”

⁶⁷ Akainua darubini juu, akaangalia, kasema, “Ndugu Branham, masalaale, ni wa kijivu!” Kasema, “Hebu mwangalie akimeremeta katika jua lile!”

⁶⁸ Nikasema, “Huyo ndiye.” Nikasema “Haya twendeni tukampate.” Kwa hiyo, hivyo ndivyo tulivyofanya, tulienda tukampata. Kulingana, katika ono, muda ulikuwa umeenda sana tusingeweza kumchinja, ilibidi tungojee mpaka kesho yake.

⁶⁹ Ndipo baada ya kumpata huyo wa rangi ya fedha, tulirudi chini, ndipo akasema, “Nawe unasema ati pembe hizo...” Kasema, “Endapo pembe hizo ni inchi arobaini na mbili, Ndugu Branham, nitazimia.”

⁷⁰ Nikasema, “Sio lazima uzimie. Lakini, ni inchi arobaini na mbili, hivyo ndivyo zilivyo.” Kwa hiyo tukafika kwenye...

⁷¹ Ndipo nikawazia, katika lile ono...Ninyi ndugu mlio inua mikono yenu, na akina dada, muda mfupi uliopita, mlionisikia nikisimulia hili kabla halijatukia. Nilisema hapana budi ilikuwa ni Billy Paul. Ilikuwa ni mvulana mdogo. Nyote mnanikumbuka nikisema hivyo, ‘mkono mdogo’? Lakini mvulana wake ana umri wa miaka kumi na minane, na kimo tu cha Billy Paul. Mnaona?

⁷² Basi nilipofika huko chini, huyo hapo Eddie amesimama amevaa shati lake la kijani kibichi lenye milia. Niliuona huo mkono mdogo ukizizunguka pembe hizo, na wakati alipoenda pale na kuchukua utepe wa kupimia, akauwekelea hapa chini, na kuushika, mvulana huyo mdogo aliweka mikono yake. Nikasema, “Angalia, Eddie, hiyo mikono midogo juu ya ile pembe.” Ndipo wakati alipouvuta huo utepe wa kupimia namna hii, aliniangalia na akawa mweupe kabisa mdomoni, akasema, “Ndugu Branham, angalia hapa! Kwenye alama kabisa, inchi arobaini na mbili, kamili!”

⁷³ Huenda ukasema, “Ndugu Branham, kwa nini unasema hivyo kwenye shule ya Jumapili?”

⁷⁴ Ninasema jambo hili kwa sababu hii. Huko nyuma kwenye Agano la Kale, wale wenye hekima na manabii wa wale waliotangulia, walimwabudu Mungu wa Mbinguni, ambaye aliwaonyesha maono. Walimpenda huyo Mungu, kwa neema Yake, ambaye aliwapenda. Waliutamani Mji mahali fulani. Kitu fulani ndani yao! Waliyaacha makazi yao nao wakawa wasafiri,

kwa kuwa walikuwa wakiutafuta Mji mahali fulani. Waliyasema mambo tunayoyaona yakitukia leo hii.

⁷⁵ Mungu yuyo huyo aliyewapenda, na kwa neema Yake, na kuwafanyia mambo hayo, ndiye Mungu yeye yule tunayemtumikia hapa kwenye maskani hii asubuhi ya leo, akifanya mambo yale yale. Na kunayo, moyoni mwetu, shauku ya Mji huo, mahali fulani ambako wamekwenda. Na kwa Neno Lake na kwa ishara za Nguvu Zake, kwa Roho yeye yule na unabii ule ule, jambo lile lile alilowafanyia huko nyuma, Yeye anatufanyia leo hii. Nanyi mnayaona kwa thibitisho lisiloweza kukosea, ya kwamba ni Mungu na Kweli ya Mungu.

⁷⁶ Kwa hiyo, popote ulipo huo Mji mkuu, na popote wamekusanyika, ninatarajia kumwona huyo mama yangu anayekufa, nanyi nyote pamoja nao, huko kwenye Mji huo ambako pamoja na hao: Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Danieli, Isaya, Yeremia. Kwa kuwa, neema ile ile ya Mungu aliyewapenda, na kuwapa maono, na kuwaonyesha mambo yajayo, ni Mungu yeye yule leo akitufanyia jambo lile lile, Kweli isiyoweza kukosea! Hiyo, ni Kweli, rafiki.

⁷⁷ Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru. Sababu ya Wewe kunitaka niypate mambo hayo, nadhani, Bwana, ulikuwa tu ukinitia moyo, ukijua kwamba kuna mshtuko unaokuja. Sijui; Wewe wajua. Nami ninajua mimi si mvulana tena. Mimi si yule mvulana mdogo aliyekuwa akishikilia nguo ya mama. Mimi ni mwanamume wa makamu sasa. Loo, jinsi ninavyokupenda, Bwana! Jinsi ninavyokuamini! Tupe neema sasa. Tusaidie kulifundisha Neno Lako, kusudi wengine wapate kuona na kujifunza, na kukujua Wewe. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁷⁸ Kwa ajili ya fungu, asubuhi ya leo. Ninafikiri hayo tu ndiyo niliyokuwa nayo, ninii tu. . . Vema, ibada usiku wa leo, ushirika, kutawadha miguu, kadhalika, hivyo tu. Nimewaalika mbaki na mwe pamoja nasi. Lakini, kwa ajili ya somo letu asubuhi ya leo, hebu tuifungue Biblia, kwenye Mathayo Mtakatifu, mlango wa 3, tusome sehemu ya Maandiko. Ninataka kuanzia kwenye kifungu cha 10 cha mlango wa 3 wa Mathayo Mtakatifu.

⁷⁹ Nami ninajua wapo wengi wamesimama, nasi tunalichukia jambo hilo; bali kama baadhi yenu mtabadilishana nao, mara kwa mara. Mimi. . . Samahani kwa kuwa, kuchukua wakati wangu, bali mimi. . . Mnaelewa. Sasa kusoma Maandiko.

. . . shoka limekwisha kuwekwa kwenye mashina ya mti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.

Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu, na kwa moto.

Ambaye pepeto lake li mkononi mwake, . . . atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.

Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana . . . ambatize.

Lakini Yohana akamzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja Kwangu?

Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Naye akakubali.

⁸⁰ Ningetaka kuchukua fungu kutoka kwenye neno hilo hapo katika kifungu cha 15.

. . . Kubali hivi sasa; kwa kuwa imetupasa kuitimiza haki yote.

⁸¹ Mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini, kwamba Yesu wa Nazareti . . . Na mara nyingi nimeulizwa. Ni kwa nini Mtu kama Yesu imbidi kubatizwa? Ni kwa nini Mtu huyu abatizwe kama tendo la toba na la maungamo, wakati Yeye alikuwa Mwana wa Mungu aliye hai, mtakatifu, asiye na mawaa, asiyeghoshiwa? Kwa nini imbidi Mtu huyu kubatizwa kama mtu anayekuja? Ubatizo ni baada ya maungamo. Hakuwa na maungamo ya kufanya, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu. Na, Yeye, ni kwa nini imbidi kubatizwa kana kwamba alikuwa nayo, “kwa toba,” kwa sababu Yeye hakuwa na haja ya toba, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu asiyeweza kukosea? “Yeye alikuwa ulimwenguni, hata kwa Yeye ulimwengu ulipata kuweko, wala ulimwengu haukumtambua.” Ni kwa nini imbidi kubatizwa?

⁸² Na je! mliona lile tamshi mbele ya jambo hilo? Lilisema:

. . . ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote.

⁸³ Kwa maneno mengine, “Haina budi kutimizwa! Neno lote alilonena Mungu, halina budi kutimizwa!” Mungu hawezi kusema lolote bila kulifanya litimie. Akiisha kulinena, ni kazi iliyomalizika. Imekwisha tayari wakati Mungu anapolinena. Mungu kamwe haneni mpaka Yeye awe tayari kwa ajili ya hilo kutimia; na, anaponena, ni kama tu limetimia tayari.

⁸⁴ Sasa, kama hilo halitapatia msingi wa kuiweka imani yetu asubuhi ya leo! Mungu anaponena Neno, limekwisha tayari. Na vipi kuhusu ahadi Zake ambazo Yeye ametupatia? Kila kitu ambacho amesema, ni kazi iliyokwisha tayari. Kwa hiyo, basi, tunapolipokea Neno Lake moyoni mwetu, ta—tayari limetimia, limekwisha!

⁸⁵ Na ni kwa nini Yeye basi (halilijibu hilo swali) abatizwe? Wengi wamesema, “Mbona, alibatizwa kwa sababu Yeye alikuwa ni mfano wetu.” Hiyo ni kweli, kwa hali fulani, mahali fulani. Hiyo ni kweli, bali siyo Kweli yote.

⁸⁶ Ukweli wake ulikuwa, ya kwamba yeye alikuwa mfano wa mfano, alikuwa ni Kuhani Mkuu. Na kabla kuhani mkuu hajatiwa mafuta, ilibidi aoshwe.

⁸⁷ Ninataka kuwasomea Maandiko fulani, kwa muda kidogo tu, kwenye Kitabu cha Kutoka. Nami nafikiri nimeandika kifungu cha 29, mlango wa 29, hasa. Nami nataka kuanzia hapa kwenye kifungu cha 4 cha mlango wa 29.

Kisha mlete Haruni na wanawe hata mlangoni mwa hema ya kukutania, ukamwoshe kwa maji.

...twaa—kisha twaa hayo mavazi na kumvika; itie kanzu, na joho...na naivera, na naivera, na kifuko cha kifuni, na kumkaza kwa huo mshipi wa naivera uliosukwa kwa ustadi;

Nawe umvike kile kilemba kichwani, na juu ya ninii takatifu...juu ya...taji takatifu utaitia katika kile kilemba.

Ndipo utakapotwaa hayo mafuta ya kutiwa, na kummiminia kichwani mwake, na kumtia mafuta.

⁸⁸ Mnaona, Haruni, kuhani mkuu, kabla hajatiwa mafuta kamwe, ilimbidi kuoshwa kwa maji. Kwa hiyo, wakati Yesu, kabla hajatiwa mafuta, Kuhani wetu Mkuu, Yeye alioshwa kwa maji.

⁸⁹ Ndipo Mafuta ya upako yakamiminwa juu Yake, kumtia mafuta. Kama vile Haruni alivyotiwa mafuta; Yeye alitiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu. “Kwa kuwa Yohana alishuhudia, akimwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, na kwenda juu Yake; na Sauti ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependezwa kukaa ndani Yake.’” Kwa hiyo Biblia ilisema ya kwamba, “Yesu alitiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, akaenda akifanya mambo mema.” Mnaona, Yeye alitiwa mafuta.

⁹⁰ Na kabla hajatiwa mafuta, ilimbidi kutimiza haki yote. Mnaona, ilimbidi kuoshwa kwa maji kabla Upako haujamshukia.

⁹¹ Na ni mfano mzuri sana wa sisi siku hizi, kama makuhani kwa Mungu. Hatuna budi kubatizwa kwanza, kuzitubia dhambi zetu kisha tubatizwe katika Jina la Yesu Kristo, tukiziosha dhambi zetu; ndipo utapokea Upako, kipawa cha Roho Mtakatifu. Mnaona, kuoshwa kwanza, kisha kutiwa mafuta kwa ajili ya huduma. Hakuna mhudumu anayepaswa kuingia mimbarani bila ya kwanza kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Maana, kuna ninii tu... Ondoleo la dhambi ni kwa Jina la Yesu Kristo pekee, la, hakuna jina lingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu. “Habari ya toba na ondoleo la dhambi haina budi kufundishwa katika Jina Lake, kuanzia tangu Yerusalemu.” Huko ndiko Roho Mtakatifu alikoshuka na kutia mafuta, kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, mhudumu ama mwaminio yeyote

hana budi kuoshwa dhambi zake kwanza, katika Jina la Yesu Kristo; kisha atiwe mafuta kwa Roho Mtakatifu, apate kutoa ushuhuda kwa ajili ya Mungu.

⁹² Naye Kristo alikuwa ni ushuhuda wa Mungu, kwa maana Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake. Sasa Yeye alisema:

...kubali hili liwe hivyo, Yohana. Hiyo ni kweli.

⁹³ Kwa maneno mengine, “Yohana, wewe ni mtu mwenye nguvu, wewe ni nabii mkuu, mwenye nguvu. Na ufunuo wako juu Yangu ni wa Kweli kabisa. Unajua kwamba Mimi ni Nani. Unajua, kwa kuwa huduma yako haikutoka kwa mwanadamu. Huduma yako ilitoka kwa Mungu. Hukuisoma kwa mwanadamu. Hukufundishwa hii katika seminari. Lakini kwenye, umri wa miaka tisa, ulienda nyikani, kwa maana ulizaliwa mtoto wa kipekee, asiye wa kawaida. Na tangu kuzaliwa kwako, Mungu alianza kukushughulikia. Na hata kabla hujazaliwa, nabii alikuona. Nawe ni nuru ya siku hii. Na huko nyikani...Wewe unajua kwamba Mimi ni Nani, kwa maana Mungu, huko nyikani, alikwambia ya kwamba kutakuwako na ishara itakayonifuata Mimi. Nawe tayari umeishuhudia, na unajua jambo hilo. Nasi tunajua sisi ni nani. Tunafahamiana. Halafu ni kweli unahitaji kubatizwa na Mimi. Lakini hebu tukubali iwe hivyo, kwa kuwa, Yohana, kama sisi ni nuru za siku hii, inatupasa kuitimiza haki yote. Neno lote la Mungu halina budi kutimizwa na sisi, kwa ajili ya siku hii, kwa kuwa imetupasa; tunapaswa, imetupasa, ni jukumu letu. Kwa kuwa kama sisi ni mashahidi wa kweli wa Mungu leo hii, Yohana, sisi ndio nuru za wakati huu. Na kama sisi ndio nuru za wakati huu, kuna Maandiko mengi sana yanayopaswa kutimizwa katika wakati huu. Na ni juu yetu!” Haleluya! “Ni juu yetu, kuona kwamba haki yote ya Mungu imetimizwa.”

Na haki yake ni nini? Neno Lake!

⁹⁴ Kwa neno lingine, “Yohana, wewe unajua kwamba Mimi ni Nani. Mimi ni Kuhani Mkuu. Hiyo ni kweli, Yohana, nami ninahitaji kubatizwa na wewe. Lakini inatupasa kutimiza haki yote. Nami ninahitaji kubatizwa na wewe. Lakini inatupasa kuitimiza haki yote. Nami nina haja ya kubatizwa na wewe sasa, kuitimiza Neno la Mungu, kwa maana Neno lote halina budi kutimizwa. Nasi ndio nuru za siku hii, na ni juu yetu kutimiza yote haya. Nami najua kwamba haki yako na shauku yako ni kuitimiza Neno. Inatupasa. Sisi ni Nuru.”

⁹⁵ Nuru ya kila wakati inapaswa kufanya jambo lile lile. Tunajua kile kinachopaswa kutimizwa. Ninyi mlio wa kiroho na mnalifahamu Neno la Mungu, mnaona kile Mungu ameahidi. Sasa Neno halitakuja kwa urahisi kamwe, bali linakuja kwa kuangaliwa, inakubidi kujitahidi kuingia ndani Yake. Lakini,

hata hivyo, inatupasa, inatupasa kuitimiza haki yote ya Mungu. Hatuna budi kuitimiza.

⁹⁶ Na sasa Yesu alitambua, katika Yohana, ya kwamba Yohana alikuwa ni nabii wa kweli. Neno lilikuwa limezungumza juu ya Yohana, na Yeye alijua ya kwamba alikuwa kabisa ndiye nabii wa wakati huo. Naye Yohana alijua ya kwamba Yesu alikuwa Masihi, wa wakati huo. Na basi wote wawili walikuwa na ufahamu mzuri.

⁹⁷ Loo, laiti Kanisa la Mungu aliye hai lingeweza kuingiza hilo vichwani mwao asubuhi ya leo, na mioyoni mwao; hata Kanisa lisingetenganishwa na vizuizi vya kimadhehebu, hizo tofauti katika kanuni za imani na rangi, na kadhalika; tupate kuungana pamoja katika Jina la Bwana Yesu, bila ya kitu chochote cha kutuondoa kutoka kwenye Neno la kweli la Mungu aliye hai; na kutembea moja kwa moja kwenye mstari huo wa Maandiko, kutimiza haki zote za Mungu za leo hii!

⁹⁸ Kwa kuwa, mtu yeyote anajua ya kwamba tunaishi katika Nuru za jioni. Nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Na kwa hiyo tunajua ya kwamba tunaishi katika wakati huo, ile saa ya Nuru za jioni. Kwa hiyo, Bwana Mungu, tusaie die kutambua jambo hilo.

⁹⁹ Hebu na turudi nyuma kidogo tu, na kuwachukua watu waliojua mahali pao katika siku yao, nao walikuwa tayari kustahimili kukosolewa ama chochote kile, kusudi Neno la Mungu lipate kutimizwa.

¹⁰⁰ Hebu tuchukue, kwa mfano, Nuhu na siku zake. Iлимпasa Nuhu, akiisha kukutana na Mungu na kufahamu mpango wa Mungu kwa ajili ya siku hiyo.

¹⁰¹ Sasa, huwezi kufanya lolote isipokuwa ujue kile unachofanya. Huna budi kujua ya kwamba ni mapenzi ya Mungu. Huna budi kujua ya kwamba ni mpango Wake na mapenzi Yake, na imefunuliwa kwako, ndipo hakuna kitu kitakachoweza kuizuia.

¹⁰² Sasa, Nuhu alijua, kwa sababu hakuwa amepata huduma yake kutoka kwenye shule fulani ya elimu, bali alikuwa amezungumza uso kwa uso na Mungu. Naye alijua ya kwamba gharika ilikuwa inakuja. Alijua ya kwamba mvua ingemwagika kutoka angani, kama mito ikifunguka, ingawa ilikuwa ni kinyume kabisa na mambo ya kisayansi ya siku hiyo. Wanasayansi, hapana shaka, walimkosoa Nuhu, na kusema, "Tunaweza kukuthibitishia kisayansi ya kwamba hamna maji huko juu."

¹⁰³ Kwa kuwa, walikuwa kwenye wakati mkuu wakati huo, mkuu kuliko tulio nao leo hii, wa kisayansi zaidi kuliko leo hii. Mnajua, Yesu alirejea kwake, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Jinsi ambavyo walijenga masfinksi na mapiramidi, na vitu ambavyo tusingeweza kuvigusa, kuvijenga

leo hii. Nao walikuwa wanasayansi mashuhuri. Walikuwa na rangi na kadhalika, na dawa za kuzuia maiti zisioze, siku hizo, hata wangeweza kufanya mumiami. Tusingeweza kufanya hivyo siku hizi hata tungefanya nini. Walikuwa na maendeleo makubwa kuliko yetu. Nao wangeweza kuthibitisha ya kwamba hakukuwako na maji kule.

¹⁰⁴ Lakini, ni mamoja, ilimpasa Nuhu, akiisha kuujuu mpango wa Mungu, ya kwamba alijenga safina, haidhuru, kwa kuwa alijua ni safina hiyo tu ingaliweza kuelea. Haidhuru, kama ilithibitishwa kisayansi ya kwamba hakukuwako na maji kule; kama Neno la Mungu lilikuwa limesema itanyesha, itanyesha.

¹⁰⁵ Na hebu nisimame hapa ili kusema jambo hili, kwa ajili ya wagonjwa. Kama wewe ni mgonjwa sana hata labda daktari anasema kwamba hakuna matumaini; hiyo inaleta tofauti gani, mradi tu Mungu anakwambia, “Nitakuacha uishi”?

¹⁰⁶ Ni kwa nini . . . Daktari ama mwanasayansi fulani angesema, “Dini yako ambayo unazungumzia, Roho Mtakatifu, na kunena kwako kwa lugha, na ninii yako—na madhihirisho yako, ni udanganyifu tu wa kimawazo.” Kwamba, “Hujajazwa na Roho Mtakatifu.” Kwamba, “Hakuna kitu kama hicho.” Na maelfu ya makasisi wanatangaza hayo leo hii, kwamba, “Umechanganyikiwa kabisa.” Kwamba, “Hakuna kitu kama hicho.”

¹⁰⁷ Na ni kwamba, baadhi yao wameniambia, “Kwa nini usijiunge na dhehebu zuri, na kutumia ushawishi wako kuliendeleza dhehebu hilo?”

¹⁰⁸ Na kisha wakasema, “Sasa, kundi hili hapa la kipentekoste unalojipumbaza nalo, hao ni kundi tu la wendawazimu wa kidini. Nao—nao . . . Hakuna kitu kama hicho. Hao wamechanganyikiwa tu kimawazo. Ha—ha—hawana kile wanachozungumzia. Tunaweza kuthibitisha ya kwamba hawana.”

¹⁰⁹ Loo, ndugu, umechelewa kupita kiasi. Tunajua kile tulicho nacho! Tumezaliwa mara ya pili, kwa Roho Mtakatifu, nasi tunaona kazi Zake moja kwa moja miongoni mwetu, kama tu ilivyokuwa katika wakati wa Biblia. Kama mnaamini katika Roho Mtakatifu yuyo huyo, basi ni kwa nini Yeye hafanyi jambo lile lile kanisani mwenu? Hakika, Yeye hawezi kubadilika; Yeye ni Mungu.

¹¹⁰ Kwa hiyo, haidhuru mathibitisho ya kisayansi yakoje, ati sisi tuna “mhemuko tu,” ati sisi “tumechanganyikiwa tu kimawazo,” ati kweli “hii dini yetu kubwa” ni bure, ati “kamwe ha—haiko vile inavyopaswa kuwa,” na kadhalika namna hiyo, ati sisi ni “kundi tu la waliotupwa nje,” msiamini hilo! Msiliamini!

¹¹¹ Kama ikitokea binti yako aje nyumbani kutoka shuleni, na kusema, “Mama, tulithibitisha, leo, ya kwamba fu—fuvu la kichwa cha binadamu ni kama tu lile la sokwe, unaona.” Ama,

“Tu—tumesoma na—na tunajua ya kwamba sote tulitoka kwenye seli moja, ya kwamba sisi ni wanyama tu.” Usiamini hilo!

¹¹² Na haidhuru mtu yeyote anasema nini, mwanatheolojia yeyote, daktari yeyote, mwanasayansi yeyote, mwalimu yeyote; wewe lishikilie tu Neno la Mungu! Kwa kuwa, kumbuka, tunajenga, kama vile, Nuhu alivyokuwa katika siku yake, tunajenga Safina.

¹¹³ Naye Nuhu alijua ya kwamba kama hakuimaliza ile safina, hata nyumba yake mwenyewe isingeokolewa. Kwa hiyo, yeye aliufahamu mpango wa Mungu. Katikati ya ukosoaji, halikumsumbua hata kidogo. Yeye alishikilia kuijenga safina hiyo.

¹¹⁴ Kwa hiyo, haidhuru ni kiasi gani wanasema, “Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.” Inatupasa, inatupasa sisi, kwamba tuitimize haki yote, kwamba tusimame katika wakati huu wa majaribu, na kushikilia kuijenga Safina ya Bwana!

¹¹⁵ Wanasema ya kwamba, “Ndugu, wewe umechanganyikiwa kabisa katika mabatizo yako, na kadhalika. Kuna . . . Hampaswi kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu.”

¹¹⁶ Nilikuwa nikizungumza na mume na mke wazuri sana jana jioni. Na kuna kijana ambaye ndiyo kwanza abatizwe, naye anaamini ya kwamba kuna Mungu mmoja tu. Na kwenye Mkutano wa Wafanya Biashara hawatamruhusu kushuhudia, kwa kuwa haamini kuna Miungu watatu.

¹¹⁷ Sasa, haidhuru wanasema nini, imetupasa, imetupasa sisi, kwamba tuitimize haki yote. Neno litabaki vile vile wakati mashirika ya Wafanya Biashara na mengine yote yamekwisha, na makanisa hayatakuwako tena. Neno la Mungu litabaki vivyo hivyo! Inatupasa kuitimiza haki yote.

¹¹⁸ Hivi manabii hawajatabiri juu ya siku hii? Kumbukeni, hao wakosoaji, inawapasa kulitimiza hilo, pia, kwa kuwa halina budi kutimizwa, pia.

¹¹⁹ Lakini, Nuhu, halikumsumbua, yeye aliendelea moja kwa moja kwa sababu aliufahamu mpango wa Mungu. Yeye alijua kile Mungu atakachofanya, Ndugu Kidd. Yeye alijua mpangilio wa Mungu kwa kuwa alikuwa amenena na Mungu, na ilikuwa ni kulingana na Neno la Mungu, naye akaendelea tu kufanya hivyo, haidhuru. Kama sayansi ingeweza kulithibitisha ama chochote kile, au ni upinzani kiasi gani uliowekwa juu ya Nuhu, yeye alidumu moja kwa moja na Neno la Mungu, na akaendelea kujenga. Kwa nini? Ilimpasa, kwa kuwa Nuhu alikuwa ni nabii. Na ilimpasa kwamba alitimize, Neno la Mungu. Alidumu nalo.

¹²⁰ Inampasa nabii yeyote, nabii wa kweli wa Mungu, kwamba adumu na Neno. Haidhuru sayansi yaweza kusema nini, na

vile *hiki* kinavyoweza kuthibitisha *hiki*, ama kadhalika, i—i— inapasa kwamba aitimize haki yote.

121 [Ndugu Branham anasoma muhtasari fulani kimya—Mh.] Vema. Walinipasha habari kumwombea mama mara moja. “Mwombee sasa. Daktari ameondoka sasa hivi.” Vema.

122 Sasa, Bwana Yesu, nimesimama hapa. Huyu ni mama yangu. Kama anatuacha, ninaiweka nafsi yake mikononi mwa Mungu. Bali huu hapa Ujumbe ambao hauna budi kutangazwa, Bwana. Wapo walio hai hapa ambao hawana budi—hawana budi kufa. Nisaidie, Bwana. Mimi ni Wako. Katika Jina la Yesu.

123 Inatupasa! Inanipasa mimi sasa kwamba niitimize haki yote. Neno la Mungu linatangulia! Hamna upendo kama upendo wa Mungu!

124 Sasa, Nuhu, haidhuru ni pingamizi gani iliyokuwa juu ya baba Nuhu, yeye alijua mahali alipokuwa amesimama, na kwa hiyo alidumu moja kwa moja na Neno. Naye akaijenga safina kwa ajili ya kuokolewa kwa nyumba yake, kwa kuwa ilimpasa kufanya hivyo. Iлимпasa Nuhu, ku—kufanya hivyo.

125 Inampasa kila Mkristo kusimama kwa Neno. Kweli kabisa. Simama kwa Neno la Mungu! Mbingu na nchi zitapita, wewe utapita, mimi nitapita, makanisa yatapita, madhehebu yatapita. Bali Neno la Mungu halitapita kamwe! Kuwa mwaminifu, msafiri mwaminifu!

126 Katika siku za Henoko, kabla tu ya ile gharika, wakati Henoko alipoangalia huko nje na kumwona Nuhu akijenga ile safina. Henoko alikuwa ni nabii. Henoko alijua ya kwamba alikuwa ni mfano. Naye alijua, ya kwamba kabla mafuriko hayajaja, ya kwamba ilimpasa kutoa mfano, kwa hiyo alasiri moja ilimpasa kwenda kutembea. Iлимпasa kufanya matembezi haya pamoja na Mungu. Na, kwa namna fulani, siku hiyo akabadilisha njia yake. Badala ya kukizunguka kilima, aliiondea Njia Kuu ya Mfalme, naye akazidi tu kutembea. “Nao hawakumwona, kwa sababu alitoweka,” bali alikuwa ameipandia Njia Kuu ya Mfalme!

127 Ee Mungu, jalia niwe kama Henoko! Wakati saa itakapofika ambapo sina budi kuondoka, jalia niipate ile Njia Kuu ya Mfalme!

128 Ninaweza kumwona Henoko. Kwa kuwa alijua ilimpasa, kwa kuwa yeye alikuwa ni nabii, naye alijua litakalotukia. Kwa hiyo, ninaweza kumwona akimpa mkewe busu la kumuaga, na kusema, “Mpenzi, nitakuona baadaye.” Akawachukua watoto wake, akawaaga kwa busu; kisha akashuka kwa mwanawe aliyekuwa ameo na binti yake aliyekuwa ameolewa, akawaaga kwa busu.

129 Wakasema, “Unaenda wapi, baba? Unaenda kutembea kidogo?”

“Naam, ninaenda kutembea.”

¹³⁰ Bali hakuchukua ile njia ya kale inayojulikana siku hiyo. Alipitia Njia Kuu ya Mfalme, ndipo akaenda Utukufuni. Ilimpasa kufanya hivyo. Hakutaka kuondoka, bali ilimpasa kuitimiza haki yote. Kwa sababu, yeye alikuwa ni mfano wa Kanisa leo hii. Alikuwa ni mfano wa Kanisa litakaloenda kwenye matembezi ya alasiri, moja ya alasiri hizi. Tutaifikia Njia Kuu ya Mfalme, nasi hao tutatoweka!

¹³¹ Naam, ilimpasa Nuhu, ilimpasa Henoko, kwamba waitimize haki yote.

¹³² Ndipo ninataka kuzungumza juu ya mtu mwingine hapa. Kulikuwa na mtu jina lake Danieli. Naye aliishi kwenye siku ya wakosoaji. Mnajua, Wana wa Israeli walikuwa wamechukuliwa kutoka katika nchi ya uenyeji wao, wakashuka Babeli, na huko walikuwa na huzuni, na kwa muda wa miaka sabini walikuwa huko. Bali kulikuwako na nabii kijana aliyeshuka pamoja nao, jina lake Danieli.

¹³³ Naye pamoja na kundi dogo, ndugu wachache tu, walikuwa wamekusanyika na kumwapia Mungu, ya kwamba hawatajitia najisi kwa ninii—kwa mielekeo mamboleo ya siku hiyo. Hawatajipumbaza na chakula cha mfalme. Hawatakunywa mvinyo wake. Hawatahudhuria karamu zake. Bali watajitakasa na kujiweka wakfu kwa Mungu, kwa kuwa iliwapasa kufanya hivyo!

¹³⁴ Ilimpasa Danieli, kwa kuwa alikuwa ni nabii, kwamba adumu na Neno.

¹³⁵ Nabii yeyote wa kweli anayelijua Neno la Mungu, ambaye . . . Endapo halijui Neno la Mungu, basi yeye si nabii wa kweli. Nabii wa kweli hudumu na Neno. Lolote Neno lisemalo, wao hudumu moja kwa moja Nalo. Haidhuru mwelekeo wa siku hiyo ukoje, ama kile ka—kanisa la kisasa lisemayo, ama yale mtu mwingine asemayo, ama mtu mwingine kufanya jambo lingine, nabii wa kweli hudumu moja kwa moja na Neno.

¹³⁶ Naye Danieli alijua, kwamba kama alidumu na Neno, kile lingemgharimu. Litamgharimu kupendwa kwake na watu. Lingemgharimu ushirika wake na ndugu wengine. Lingemgharimu mambo mengi sana. Lakini walitoa hoja, kwamba, watamwabudu mungu fulani, halafu baadaye wangerudi na kumwabudu mungu yeyote.

¹³⁷ Lakini mnajua, jambo fulani kuhusu Hilo, Mungu, hatupatani juu ya Mungu. Hakuna kupata- . . . kupatana, juu ya Mungu. Mungu hudumu tu Mungu! Yeye hatutarajii, Jumapili, kuwa Wakristo, tukimsifu na kumwabudu; na, Jumatatu, vivi hivi na kulishusha, na kila namna ya mawazo, kwamba, “Labda nilikosea, nami ilinipasa kufanya *hivi* ama *vile*.” Tunakaa tumeelekeza macho yetu kwenye Neno la Mungu, na kukaa moja kwa moja Kwake!

¹³⁸ Kwa hiyo tunaona ya kwamba, Danieli, ilimpasa, kama nabii, kudumu na Neno, haidhuru! Kwa hiyo kulitolewa tangazo, nalo likasema, “Ya kwamba yeyote atakayemwabudu mungu mwingine yeyote, mbali na mungu waliyekuwa wamemchagua.” Kwa maneno mengine, “Usiposhirikiana nasi, tutakutupa tu kwenye tundu la simba.” Vema, ilimpasa Danieli, ilimpasa yeye kuitimiza haki yote, kwamba hatamwabudu mungu mwingine yeyote, wala kujizongazonga na mambo ya ulimwengu; ni kwa Mungu pekee! Kwa hiyo, yeye alifungua tu madirisha na kuliinua dirisha, kisha akafungua mapazia, na kuuelekeza uso wake Mashariki, na kuomba mara tatu kwa siku, kama tu alivyofanya daima. Kwa nini? Sio kwenda kifichifichi mahali fulani na kujificha, kufanya hivyo, bali aliyafungua madirisha wazi; mtu yeyote apate kuona, anayetaka kuona. Hakuionea haya dini yake.

¹³⁹ Kwa sababu, inakupasa Mkristo usiionee haya dini yako. Kama vile Paulo, wa kale, alivyosema, “Kwa njia ile ambayo waiita uzushi, wenda wazimu, ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu.” Mnaona? “Siionee haya Injili ya Yesu Kristo,” yeye alisema, “kwa kuwa ni Uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aiadiniye.” Hiyo ni kweli, kutokuionea haya Injili! Ndicho kitu kinachoshikilia katika wakati meli inapoyumbayumba na kila nyota haionekani, na mwezi na nyota, na dhoruba zinavuma. Ingali inashikilia, kwa maana ni Injili ya Yesu Kristo!

Danieli alikuwa ni mwaminifu. Ilimpasa.

¹⁴⁰ Wana wa Kiebrania, iliwapasa, iliwapasa wao, wakiisha kuchukua msimamo wao kwa ajili ya Mungu. Iliwapasa. Hawakujali juu ya tanuru ya moto. Chini ya majaribu magumu, walijali nini? Walikuwa wamechukua msimamo.

¹⁴¹ Ee Mungu, laiti Wakristo wa siku hizi wangeliona jambo hilo! “Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Nimeanza pamoja na Yesu, Ee Bwana, nichukue, nifanikishe.” Chini ya jaribu, shida, huzuni, mauti, maradhi, majonzi, ningali nitasimama pamoja na Yesu Kristo, kuuchukua msimamo wangu! “Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama, sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.” Kila kitu kingine kinazama. Falme zitaanguka, na mataifa yatavunjika, na madhehebu yatatawanyika, na wanatheolojia watakufa, bali Neno la Mungu, daima litabaki vile vile!

¹⁴² Naam, iliwapasa kuchukua msimamo wao. Na iliwapasa, baada ya kuchukua msimamo, kwamba waudumishe msimamo wao.

¹⁴³ Unapokuja asubuhi ya leo, ukiamini ya kwamba Mungu atakuponya, nawe uchukue msimamo wako, inakupasa kwamba usishuhudie kinyume na huo; la sivyo, usije. Hiyo ni kweli. Kama

hujisikii kana kwamba Mungu angekuponya, basi kaa mbali, unalifanyia dhahaka tu.

¹⁴⁴ Kama ukijisikia, asubuhi ya leo wakati wito wa madhabahuni utakapokuja, ya kwamba, “Ninataka kuchukua msimamo wangu kwa ajili ya Kristo.” Kama ukijisikia, hesabu gharama; wahesabu watu wako, uone kama unaweza kwenda vitani. Angalia kama uko tayari. Usipojisikia kama uko tayari, usije. Lakini kama kitu fulani kinakwambia, “Hii ndiyo siku yangu, hii ndiyo asubuhi yangu,” basi utakuja na ubaki hapo daima! Kamwe usisogee, haidhuru kama mauti yanakukabili, na ukungu unaelea usoni mwako. Unajali nini? Simama pale! Kwa kuwa, “Mbingu na nchi zitapita; Maneno Yangu hayatapita kamwe!” Utadumu Nalo.

¹⁴⁵ Unaposema, “Ninamwamini Yesu Kristo kama Mponyaji wangu. Ninaamini, asubuhi ya leo, ya kwamba Yeye atakuponya mwili wangu mgonjwa. Kitu fulani kiliniambia niye kanisani. Nipo hapa miongoni mwa waaminio. Ninauchukua msimamo wangu, asubuhi ya leo. Ninaliamini! Nitaombewa. Nitakapombewa, nitabaki hapo kwenye msimamo huo! Haidhuru kuna giza jinsi gani, ama iko wapi, ningali nitasimama kwenye msimamo huo.” Ulichukua msimamo huo kwa sababu inakupasa.

¹⁴⁶ Ukiisha kuungama, inakupasa kudumisha maungamo yako. Hiyo ni kweli. Inakupasa, kama Mkristo, kama mwaminio, kudumisha imani yako.

¹⁴⁷ Usimruhusu ibilisi akusukume *huku* na *huko*. Daima umechanganyikiwa. Daima umetoka kwenye barabara kuu. Daima unaingia na kutoka. Na hivyo ndivyo huwezi kukaa popote. Huwezi kuwa na imani kwa nafsi yako. Ama, huwezi, hakuna mtu anayeweza kukuamini. Inakupasa kusimama! Na ukiisha kufanya yote uwezayo kufanya ili kusimama, basi simama! Endelea tu kusimama! Hiyo ni kweli. Hatuna budi kufanya hivyo. Inatupasa. Inatupasa sisi, kwamba tufanye hivyo.

¹⁴⁸ Ilimpasa Eliya, ilimpasa Eliya nabii, kwamba achukue msimamo wake kulitimiza Neno la Mungu, kwa kuwa alilifahamu Neno la Mungu. Naye alijua ya kwamba huyu askofu mkuu, Yezabeli, na tofauti zao zote za kimadhehebu zilichanganyikana na mwelekeo wa ulimwengu. Ilimpasa Eliya, kama nabii, kwamba asimame. Naye akasimama peke yake! Kamwambia Mungu, “Wote wameondoka, ila mimi, nami ninasimama peke yangu.” Hiyo ni kadri alivyojua. Mungu alisema alikuwa na wengine zaidi waliokuwa wamechukua msimamo uo huo; labda si katika mahali a—alipokuwa Eliya, kwa kuwa alikuwa amelengwa na taifa. Hao hawakupata pingamizi kama alizopata, kwa kuwa wote walikuwa wakimlenga, kwa sababu yeye alikuwa ni nabii. Lakini ilimpasa,

katikati ya majaribu, kati ya pingamizi, kati ya kutojali; ilimpasa Eliya, kama nabii, kumtetea Mungu, na kusimama hapo.

¹⁴⁹ Inatupasa kuitimiza haki yote. Wale watu wakuu, wenye nguvu, wakionyesha mfano wa siku hizi ambapo dini ya Yezebeli na kadhalika inainuka sasa, mambo tuliyo nayo siku hizi, ikijaribu kuchukua mamlaka. Inampasa mtumishi wa Mungu, haidhuru mtu yeyote anasema nini ama ni kitu gani kinachotukia, kusimama, kwa kuwa imetupasa kudumu na Neno.

¹⁵⁰ Eliya alijua alikuwa ni nabii. Aliona maono. Mungu alikuwa amenthibitisha kwamba ni nabii. Kwa hiyo haidhuru kama ndugu zake. . . Kulikuwako na makumi elfu; hebu waangalie tu Israeli, wakiwa mamilioni, watu waliodai kumwamini Yehova, walikuwa—walikuwa wamejiundia madhehebu. Walikuwa wamekuwa wa kisasa, kama walivyo leo hii. Walijifanya wa kisasa. Walipatana katika Neno Lake. Haleluya, bali ilimpasa, Eliya, kwamba atimize haki yote. Kwa hiyo alisimama pale, peke yake, akiyakemea maovu! Kama wangaliyachukua maisha yake, vipi basi? Ilimpasa, kuitimiza haki yote. Kulikuwa na maovu nchini. Kulikuwa na kutojali nchini. Kulikuwa na mambo maovu kimaandiko nchini. Na ilimpasa Eliya, kuitimiza haki yote, kumtetea Yehova; ndipo Yehova akamtetea Eliya. Amina. Ilimpasa!

¹⁵¹ Ibrahimu. Ilimpasa Ibrahimu kujitenga na kutokuamini. Inampasa mwaminio yeyote kujitenga na kutokuamini! Ibrahimu, ilimpasa kutembea katika nchi yake mwenyewe, yeye na Mungu, pekee, maana alikuwa ni nabii. Ulimwengu haukuelewa ni kwa nini Ibrahimu alifanya chaguo kama hilo. Ni kwa nini akaondoka nyumbani mwake? Ni kwa nini akaliacha kanisa lake? Ni kwa nini akawaacha watu wake? Ni kwa nini akafanya jambo la kijinga kama hilo, kuwa mgeni katika nchi ya kigeni ambamo hamna maji wala chakula? Ni kwa nini akaenda kwenye majangwa hayo yenye ukiwa jinsi hiyo ambamo binadamu walikuwa hawajafika huko bado? Lakini ilimpasa, kwa kuwa yeye alikuwa ni nabii, kujitenga na kutokuamini kote, na kutembea peke yake pamoja na Mungu. Mungu alisema, “Jitenge, nami nitakubariki.”

¹⁵² Unapojitenga na kutokuamini kote, Mungu atakubariki. Na inampasa kila mmoja wetu, haidhuru itagharimu nini, kujitenga na ulimwengu usioamini. “Ondokeni kwao, mkatengwe nao,” asema Mungu, “nitawapokea.” Inatupasa, kama wanaume na wanawake wa Mungu, kuchukua msimamo wetu katika saa hii yenye giza tunayoishi.

¹⁵³ Ibrahimu, bila kujali wengine wao waliwazia nini, alijitenga. Kwa nini? Alikuwa amemwona Mungu. Aliona ono. Ono hilo lilikuwa ni la kweli, ono hilo lilitimia. Alijua Mungu

alikuwa pamoja naye; Ibrahimu, kutoa tamshi la kijinga kama alilotoa. Mtu mwenye umri wa miaka mia moja, naye mkewe tisini, naye mke alikuwa ni tasa naye mume mgumba, nao walikuwa watampata mtoto kwenye umri huu. Mbona, sayansi ya matibabu ya wakati huo ingemwita namna fulani ya mpotovu. Wangalimwita “mwendawazimu.” Lakini ilimpasa. Haleluya!

¹⁵⁴ Wakati mwingine inapasa kuwa mpotovu, kama ni kulingana na Neno.

Mungu alikuwa amenena naye, kasema, “Ibrahimu.”

Kasema, “Naam, Bwana?”

¹⁵⁵ “Mimi ni Mungu wa baba zenu. Mimi ni Mungu wa Umilele. Mimi ni El Shaddai; Mimi ni Kifua, Mimi ni Titi, Mimi Ndimi Mpaji-Nguvu. Sijali wewe ni mzee jinsi gani, Ibrahimu, hiyo ni nini Kwangu? Sijali jinsi ulivyo mgumba ama jinsi tumbo lake lilivyo tasa, nitakupa mwana.”

Naye Ibrahimu akasema, “Ninakuamini, Mungu.” Haleluya!

¹⁵⁶ Biblia ilisema, “Hakusita kwenye ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu.” Kwa nini? Ilimpasa. Alikuwa ameuona mkono wa Mungu ukitenda kazi, katika nguvu.

¹⁵⁷ Loo, Maskani ya Branham, tutatoa neno la namna gani kwenye ile Siku ya Hukumu? Wakati, tumeuona mkono Wake wenye nguvu. Tumeziona Nguvu Zake. Tumeutazama Utukufu Wake. Tumeona yale aliyosema; hayashindwi kamwe. Tumeuona Utu Wake, ile Nguzo Kuu ya Moto, Nuru inayoning’inia humu chumbani. Tumeiona huko ng’ambo, sayansi imeipiga picha, na kila kitu. Pia tumeusikia Ujumbe ukitolewa, moja kwa moja mstarini, “Jitengeni nao! Msihusike na chochote cha kutokuamini!” Imetupasa, kwamba tuitimize haki yote.

¹⁵⁸ Ibrahimu alikiri alikuwa ni msafiri na mgeni. Hakuwa na la kufanya; hakumjua mtu yeyote duniani. Alitembea na Mungu, kwa sababu ilimpasa, kwa kuwa alikuwa amemwona. Ilimpasa Ibrahimu. Wakati wafalme hao wote walipokutana huko nje, mwajua, kumfanya mtu mashuhuri; wafalme wote, baada ya Ibrahimu kupata ushindi huu mkuu, wakati hao wafalme walipokutana naye huko, ndugu wote wa kimadhehebu, na kusema, “Unajua, Ibrahimu, tuta—tutafanya mapatano na wewe. Tutafanya *hivi na hivi*.”

¹⁵⁹ Akasema, “Sitajichukulia hata kamba ya viatu, mimi; usije ukasema, ‘Nilimfanya Ibrahimu kitu fulani.’”

¹⁶⁰ Loo, ilimpasa, kwa kuwa alijua (Haleluya) ya kwamba Mungu alimwapia, “Nitakupa kila mahali utakapoangalia: mashariki, kaskazini, magharibi, ama kusini.”

¹⁶¹ Inaleta tofauti gani kama tuna ndururu ama senti moja, kama tuna chakula ama hatuna, kama tunaishi ama tunakufa? Mungu aliahidi, “Wenye upole watairithi nchi.” Inatupasa,

inatupasa sisi, kwamba tuishi hivyo, tutende hivyo, inatubidi kutimiza haki yote. Mungu anawataka wanaume na wanawake ambao watasimama na kutimiza haki yote! Bila shaka, *haki* ni “Neno Lake.”

¹⁶² Kama nilivyosema mwanzoni mwa mahubiri, hiyo ndiyo sababu Yesu alibatizwa. Haidhuru ilikuwa jinsi gani. . . Kama Yeye alidai kuwa ni Mwana wa Mungu, halafu abatizwe, kwa ondoleo la dhambi? Hakuwa na yoyote. Lakini ilimpasa kuoshwa, kwa sababu Yeye alikuwa ni Kuhani Mkuu. Iлимпasa kuitimiza haki yote. Kasema, “Kubali iwe hivyo, Yohana. Ninajua unajua jambo hilo. Ninajua ya kwamba ninalijua. Nasi tunafahamiana. Lakini tutakubali hiyo iwe hivyo, bali inatupasa.” Amina! Haleluya!

¹⁶³ Basi nitaambatana na wachache wa Bwana waliodharauliwa! Inanipasa, inawapasa ninyi, kama watumishi wa Mungu, kwamba tuambatane na wachache wa Bwana waliodharauliwa; kwamba tutembe kitauwa, wenye haki, watakatifu, katika maisha haya ya sasa; tukiweka kando kila mzigo utuzingao kwa upesi; tukimtazama Mwenye Kuanzisha na Mwenye Kutimiza imani yetu, Yesu Kristo! Amina.

Iлимпasa Ibrahimu, wakati alipokwea kule juu.

¹⁶⁴ Ndipo Mungu akamwambia, “Sasa, mchukue mvulana huyu mdogo. Sasa wewe una umri wa (kadiri ya) miaka mia moja na ishirini. Nawe una mvulana mdogo hapa, maskini mwenye nywele za kipilipili. Yeye ni kipenzi kidogo. Lakini ninataka umpandishe huko juu ya mlima, nawe umtoe sadaka, kwake yeye nitafanya mataifa mengi kutoka kwako.” Ingewezekanaje? Ilionekana kana kwamba Mungu alichanganyikiwa kabisa. “Nitachukua, kwa njia ya Isaka, na kuubariki ulimwengu mzima na kila taifa, pamoja naye; lakini ninakutaka, umchukue umpandishe huko juu na kumwua. Kupitia uzao wa Isaka. . .” Haleluya! “Kupitia uzao wa Isaka nitalibariki kila taifa chini ya Mbingu, bali ninataka umpandishe kule ukamwue.”

¹⁶⁵ Loo, huyo baba mkongwe, mkali, shupavu; amebeba kuni na gunia mgongoni mwake, akimwongoza punda. Jamani! Maskini Isaka akitembea mbele zake! “Hakusita kwenye ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini.” Iлимпasa!

¹⁶⁶ Kwa kuwa Ibrahimu alisema, mwenyewe, “Nilimpokea kama aliyetoka kwa wafu, nami nimeshawishika kabisa ya kwamba Mungu anaweza kumfufua tena.” Amina! Iлимпasa Ibrahimu, kuitimiza haki yote. Yeye alijua alichokuwa akinena habari zake. Alimjua Mungu wake. Alijua, yale Mungu aliyosema, Mungu anaweza kutimiza. Ile ahadi aliyofanya Mungu, Mungu anaweza kuitimiza ahadi Yake, haidhuru. Kwa hiyo, ilimpasa Ibrahimu kwamba atimize haki yote.

¹⁶⁷ Iliwapasa wanafunzi, kwenye Pentekoste, wapande kwenye hicho chumba cha juu. Kwa nini? Ni kwa nini iliwapasa?

Kwa sababu walikuwa wamekutana na Mtu; Seremala, aliyejulikana kwa ulimwengu, Mgeni wa Galilaya aliyekuwa na jina baya, “mwana haramu.” Lakini walikuwa wamemwona mtu huyo akiwafufua wafu. Walikuwa wamemwona Mtu huyo akiyafungua macho yaliyopofuka. Walikuwa wamemsikia Mtu huyo akihubiri Neno la Mungu, lisiloghoshiwa. Nao walijua alikuwa ni Masihi. Walikuwa wameona ishara zote alizokuwa nazo. Walikuwa wamemsikia Mungu akijibu kutoka Mbinguni. Walikuwa wameiona ile Nguzo ya Moto ikining’inia juu yake. Walijua Yeye alikuwa ni Masihi. Ndipo wakati alipowaambia, “Yafaa Mimi niondoke; bali ninawataka mpande mwende kule kwenye mji wa Yerusalemu, na mkae kule. Ngojeni tu kule.”

“Kwa muda gani?”

“Mpaka!”

“Hiyo itachukua muda gani, Bwana?”

¹⁶⁸ “Mpaka tu! Mpaka mtakapovikwa Nguvu zitokazo Juu! Ndipo mtakuwa mashahidi Wangu.”

“Itachukua muda gani, Bwana?”

¹⁶⁹ “Kwa kizazi *hiki*, na kwa kizazi *kile*, na wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Huko Yerusalemu, Judea, Samaria, na pande za mwisho za dunia. Lakini, kabla hamjaenda, ninawatakeni mngoje! Nitawafanyia jambo fulani.”

¹⁷⁰ Iliwapasa kwamba waende kwenye chumba cha juu, kwa sababu walikuwa wameziona Nguvu Zake. Wanajua ya kwamba Yeye alikufa, amekufa. Alikufa akawa mfu sana hivi kwamba hata mwezi na nyota zikashuhudia ya kwamba alikuwa amekufa, zikaficha nyuso zao hata zisingeangaza. Dunia ilijua kwamba amekufa mpaka ikatikisika kwa unyong’onyevu wa neva. Miamba ilifoka kutoka ardhini, ambayo ilikuwa mle ndani tangu siku zilizotangulia ule uharibifu wa gharika. Walijua huyo alikuwa ni Masihi. Walijua hivyo, Neno Lake lilikuwa, ya kwamba atamrudisha Roho Mtakatifu. Walijua hiyo ilikuwa ni ahadi. Walijua ya kwamba iliwabidi kumngojea kule juu. Walikuwa wamemwona. Walijua alikuwa amekufa; walijua alikuwa amefufuka. Walikuwa wamemwona, kwa hiyo walijua kile walichokuwa wakizungumzia.

¹⁷¹ Mpaka mtu ajue kile anachozungumzia, hawezi kusema mengi sana. Ila unapojua unalozungumzia! Endapo unafikiri huu ni mhemuko, njoo uupate wakati mmoja, ndipo utajua kile unachozungumzia. Si mhemuko. Ni Nguvu za Mungu ziletazo wokovu. Ni Roho Mtakatifu. Ninajua yale ninayozungumzia. Kila mmoja, aliyempokea, wanajua kile wanachozungumzia.

¹⁷² Iliwapasa wanafunzi, iliwapasa kulitimiza Neno Lake, kungojea huko Yerusalemu. Kwa hiyo walipanda wakaenda kungojea huko Pentekoste, mpaka wakampokea Roho Mtakatifu. Kwa kuwa, ndipo walijua ya kwamba huduma yao

isingeweza kuendelea mpaka walipompokea Roho Mtakatifu, kumshuhudia. Walijua hawajiwezi. Bali iliwabidi kuwa na Uwepo Wake, kwa hiyo wakaenda kumngojea.

Iлимпаса Петро, baada ya Yesu kukutana naye.

¹⁷³ Katika Marko 16, ilisema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watachukua nyoka; watakunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

¹⁷⁴ Iлимпаса Mtakatifu Петро, yule mvuvi mkongwe, hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mweyewe. Lakini siku moja wakati alipokuwa akipitia kwenye lango Zuri ambalo Sulemani alikuwa amelijenga, pale alilala kiwete. Magoti yake yalikuwa ni dhaifu, vifundo vyake vya miguu, asingeweza kutembea. Alikuwa jinsi hiyo. Hakuwa na nguvu. Mtu mwenye umri wa yapata miaka arobaini, wala hakuwa na nguvu. Lakini wakati Петро aliposikia kikombe kikichacharika, naye akaangalia chini akamwona kiwete amelala pale, ndipo kitu Fulani kiliugongagonga moyo wake kwa nguvu! Alikuwa huko Pentekoste, alikuwa na Roho Mtakatifu! Alikuwa na ahadi ya Yesu, kwa hiyo ilimpasa, ilimpasa yeye, hata akasema, “Sina fedha wala dhahabu.” Akatoa ushuhuda wake, “Sina fedha wala dhahabu. Lakini, nilicho nacho, nitakupa kama unaweza kukipokea.”

Ninaweza kumwazia mtu huyo akisema, “Ninaweza kukipokea.”

¹⁷⁵ Kasema, “Basi, katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama kwa miguu yako upate afya.” Basi akainama akamshika, apate kuitekeleza imani yake, na kumwinua namna hiyo; ndipo mifupa ya kifundo chake ikapata nguvu, naye akaenda, akiruka, akimsifu na kumtukuza Mungu.

¹⁷⁶ Iлимпаса kufanya hivyo, ilimpasa. Alipaswa kufanya hivyo, kwa kuwa alikuwa ni mwanafunzi aliyetiwa mafuta. Alishakuwa pamoja na Yesu. Ulimwengu mzima ulijua, siku moja kabla, kwenye Baraza la Wazee, walipowakusanya, yeye na Yohana, wote wawili, wasio na elimu wala maarifa; walijua walishakuwa pamoja na Yesu, maana waliwasikia jinsi walivyokuwa wakizungumza, ujasiri waliokuwa nao. Walijua kwamba jambo fulani lilikuwa limewapata. Naye Петро alijua hilo. Kwa hiyo ilimpasa Петро, ilimpasa kwa kuwa alikuwa na ahadi ya Mungu kwa ajili ya siku hiyo.

¹⁷⁷ “Nitawapa Nguvu. Nitawapa Nguvu. Mtavikanyaga vichwa vya nyoka na nge. Lolote mwombalo katika Jina Langu, hilo nitalifanya. Mkiuambia mlima huu, ‘ng’oka,’ wala msitie shaka moyoni mwenu, bali muamini ya kwamba mliyosema yatatimia, yatakuwa yenu.”

178 Inampasa Petro basi kuliadini. Inampasa. Hivyo ndivyo anavyopaswa kufanya, kwa sababu yeye alijua aliishi katika siku ya hilo agizo. Hiyo ilikuwa ndiyo Nuru ya wakati huo. Ule ufufuo ulikuwa ndio tu umekuja, Roho Mtakatifu alikuwa hapo. Iimpasa.

179 Iimpasa Mtakatifu Paulo; baada ya kuwa mpinzani. Na akienda zake Dameski, siku moja pale, Nguzo ile ya Moto ambayo ilikuwa imewaongoza Israeli kutoka Misri kuingia kwenye nchi ya ahadi, ambayo ilikuwa imefanyika mwili ikakaa miongoni mwao kisha ikarudi kwa Mungu, ilisema naye. Naye akashangaa, “Ingewezaje hii kuwa ni Yehova? Ingewezekanaje? Naye yule pale, katika Nguzo ile ile ya Moto, ikining’inia pale.” “Bwana, U nani Wewe ninayemtesa?”

180 Akasema, “Mimi ni Yesu.” Loo, jamani! Yeye alimwagiza, akampa huduma yake. Akamwagiza Paulo, akampa huduma yake.

181 Paulo alikwishakuwa katika Uwepo wa Mungu, alikuwa ameiona ile Nguzo ya Moto. Alimwona yule Yesu ambaye wakati mmoja alikuwa ni Nguzo ya Moto, kisha akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu, kisha akarudi kuwa Nguzo ya Moto, na kumwagiza katika huduma yake. Haleluya! Hakuna kitu kitakachomtikisa. Iimpasa, wakati walipotoa lesa mwilini mwake na kuwapelekea wagonjwa. Iimpasa, kwa kuwa yeye alijua alikuwa ni mtume aliyetiwa mafuta. Aliona maono ya Mungu, Naye Mungu akamtokea na kunena, na kuliona likitukia vivyo hivyo hasa. Mbona, iimpasa Paulo, kwamba wakati alipojaribu kuwasaidia watu, kulitimiza Neno aliloagizwa. Yeye alikuwa ni Nuru ya siku hiyo. Alikuwa ni Nuru ya Mataifa. Alijua hilo. Mungu alimwagiza kuwa. Alikuwa Nuru katika siku hiyo. Kwa hiyo, aliagizwa kwa Paulo.

182 Sasa inatupasa, inatupasa katika siku hii. Tunajua! Ndiyo kwanza tu tupitie kwenye Nyakati za Kanisa. Tunajua ya kwamba tumempokea Roho Mtakatifu, tunajua hilo pasipo tashwishi. Tunajua tunayo Nuru ya Injili.

183 “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Hakuna kasisi ulimwenguni, ama yeyote yule, anayeweza kukanusha hilo. Hili linapaswa kufanyiwa umbali gani? “Ahadi hii ni kwa ajili ya watoto wenu, kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

184 Nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni, Nuru hizi za Injili zitarudi tena.” Kama vile jua lile lile linavyochomoza Mashariki na kutua Magharibi, litarudi tena katika siku za mwisho. Sisi hapa katika siku za mwisho!

185 Tumempokea Roho Mtakatifu. Tunajua hilo. Tulisema kwa lugha kama walivyofanya kwenye Pentekoste. Nasi tunajua mnaweza kumpokea.

186 Tunajua ya kwamba malaika wa saba ameutoa Ujumbe. Tunauona ukithibitishwa, ile ishara.

187 Tunajua ya kwamba tuko mwishoni mwa Wakati wa Laodikia. Tunajua ya kwamba ugomvi wa kitaifa, ishara na maajabu, zinatokea kila mahali. Tunajua ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

188 Mungu akishuhudia! Nayo inatupasa, inatupasa sisi kwamba tuitimize haki yote. “Mataifa dhidi ya mataifa, mshangao wa wakati, dhiki,” mambo haya yote ambayo tumesikia. Kama mnaweza kulipokea!

189 Sasa tuko kwenye saa ya mwisho. Tuko kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia. Kila mjumbe ameutoa wakati wake, ametoa Ujumbe wake katika wakati wake. Nasi tuko hapa kwenye mwisho wa wakati, nasi tunaona ya kwamba Mungu amelithibitisha kwa ishara na maajabu. Wala hakuna mtu anayeweza kusema sivyo ilivyo.

190 Yeye yupo hapa sasa! Yeye yumo Kanisani! Yumo ndani ya watu. Hakuna mtu anayeweza kusema sivyo ilivyo. Tunajua ya kwamba Yeye yupo hapa.

191 Basi inatupasa kulichukua Neno Lake. Sisi, inatupasa kuamini haki yote. Inatupasa. Imetupasa kwamba tutimize kila kitu alichozungumzia.

192 Kanisa ni dhaifu, makanisa ya siku hizi. Tumegawanyika katika ugomvi wa kimadhehebu, utengano wa ndugu; Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Umoja, Utatu, Utano, kila namna ya upuuzi. Tumegawanyika. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Haina budi kuwa hivyo.

193 Ndipo utakuja Ujumbe! Loo, Haleluya! Tunajua ya kwamba ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza Israeli. Tunajua kwamba huduma ile ile iliyoambatana na Yesu Kristo, kwa Nguzo ile ya Moto iliyomtia mafuta, inaambatana na Kanisa leo hii. Sayansi imelithibitisha; hatuhitaji hilo. Mungu amelithibitisha! Tunahitaji huduma ya Yesu Kristo ipate kuenea kwenye lile Jiwe la Kuweka Juu linalokuja huko, ambalo limelifikisha kanisa mahali ambapo huduma hii imefanana kabisa na wakati Yesu alipoondoka. Kabisa!

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara zilizotabiriwa na watu wenye hekima;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
“Rudini, makwenu, enyi mliotawanyika.”

194 Tuko katika siku za mwisho. Na inatupasa, inatupasa sisi kwamba tutimize haki yote.

195 Kumbukeni, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Ni wangapi wanaokumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Ilikuwa katika siku za Lutu? Yeye alitoa ishara gani?

196 Kulikuwako na matabaka matatu ya watu katika siku za Lutu. Hiyo ilikuwa ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kulikuwako na asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio. Kila mmoja wao alipokea mjumbe. Hiyo ni kweli. Wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi chini ya mwaloni wake, ni kitu gani kilitukia? Angalia kilichotukia.

197 Kuna Malaika aliyeshuka akaenda Sodoma. Mtu huyu alishuka kule na kuwafundisha toba, ya kwamba inawapasa kutubu na kumrudia Mungu. Ni jambo gani lililotukia? Ni watatu tu waliotoka, Lutu na binti zake wawili. Mke wake aligeuka nguzo ya chumvi. Ni watatu tu waliotoka, ambapo kulikuwako na Billy Graham wa kisasa aliyewarushia ujumbe mle ndani.

198 Nasi tunaona hilo likitendeka leo hii. Tunaona, kwa kanisa la kawaida, tunamwona mjumbe anatokea, akihubiri.

199 Pia kulikuwa na Mmoja aliyemjia Ibrahimu na Kanisa lililoteuliwa. Yeye aliwapa ishara. Nasi tunajua hilo ni kweli. Tunajua kwamba ni kweli. Yeye aliketi ameelekeza mgongo wake kwenye hema, akamwambia Sara alikuwa ni nani, kilichokuwa moyoni mwake, shida yake ilikuwa ni nini. Alitoa ujumbe, hakika. Ibrahimu alijua huyo alikuwa ni Mungu. Kwa kuwa, mara baada ya Yeye kusema hivyo, alimwita, “Elohimu,” Mjumbe, aliyefanywa katika mwili wa mwanadamu, kuuleta Ujumbe Sodoma na Gomora.

200 Basi tunapoyaona mambo hayo ambayo Yesu alisema yangetimia, inatupasa kutimiza haki yote. Inatupasa kwamba tumwamini Mungu kulingana na Neno Lake. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi kubali iwe hivyo sasa.

201 “Ndugu Branham, wewe—wewe—wewe huendani na hayo mengine, madhehebu.”

202 Huenda hilo likawa ni kweli. Kubali iwe hivyo sasa. Hiyo ni kweli, kubali iwe hivyo.

203 “Vema, ingekufaa sana kama ungeendelea na kushirikiana.”

204 Kubali iwe hivyo sasa, hilo. Lakini inatupasa. Sisi ni watu Wake, manabii Wake, wenye hekima Wake. Inatupasa tutimize haki yote. Kwa hiyo, hebu na tufanye hivyo, tunapoviinamisha vichwa vyetu.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia imetabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;

“Rudini, makwenu, enyi mliotawanyika.”

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zisafishwe na ziwe
safi,

Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

Manabii wa uongo wanadanganya, Kweli ya
Mungu wanaikana,

Ya kwamba Yesu Kristo Ndiye Mungu wetu,
(Jinsi hilo lilivyo kweli; loo, mamia!)

Bali tutatembea ambapo mitume
wamekanyaga.

Kwa kuwa siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zisafishwe na ziwe
safi,

Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

²⁰⁵ Wakati mmeviinamisha vichwa vyenu, je! inakupasa, asubuhi ya leo, kwamba uyatoe maisha yako kwa Kristo? Amesema nawe? Kama ndivyo, mwinulie tu mkono wako, na useme, “Sasa ninamkubali Kristo. Inanipasa nitoe yangu yote, mapenzi yangu, asubuhi ya leo, Kwake. Sasa ninauinua mkono wangu na kusema, ‘Bwana Yesu, unirehemu.’ Nakuhitaji, loo, jinsi ninavyokuhitaji! Kila saa, nakuhitaji.” Mungu awabariki. “Loo, Mwokozi Mbarikiwa, naja Kwako.”

Nakuhitaji, loo, nakuhitaji;

Vipi kama ulikuwa umelala mahali mama amelala sasa?

Kila saa nakuhitaji!

Loo, nibariki sasa, Mwokozi wangu,

Naja Kwako!

[Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

(Ee Bwana, tunakuhitaji;)

Nakuhitaji kila saa!

Loo, nibariki sasa,

Bwana, ninakuhitaji sasa kuliko vile nimekuhitaji muda mrefu.

Ila naja Kwako!

²⁰⁶ [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, *Nakuhitaji Kila Saa*—Mh.]

²⁰⁷ Baba wa Mbinguni, chini kupitia mabondeni tunatembea, tukijua ya kwamba Wewe umeahidi, “Sitakuacha, wala

sitakupungukia. Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake, hayo mengine yote mtazidishiwa.”

Kwa hiyo naja kwako!

208 Kama kukiweko na mmoja hapa, Bwana, ambaye si sawa nafisini mwao; kama walikuwa wakishuka kwenye kinjia kile, alimo mama yangu dakika ii hii, Ee Bwana, jalia wawe na ushuhuda huo, pia. Inatupasa leo hii, Bwana.

209 Tuko kwenye mwisho wa safari, Wakati wa Kanisa la Laodikia; Ujumbe; kule kukataliwa kwa Ujumbe; kule kuthibitishwa kwa Ujumbe; na Uwepo wa Kristo ukithibitisha ni yeye yule, jana katika siku za Lutu, na katika siku za mwili Wake, na katika siku za leo hii; jana, leo, na hata milele.

210 Jalia wakupokee sasa kama Mwokozi wao mbarikiwa. Tujalie, Bwana. Ninaomba katika Jina la Yesu.

Loo, nibariki sasa, Mwokozi wangu,
Naja Kwako!

Bwana wa thamani sana,
Majaribu hupoteza nguvu zao,
Hakika, Bwana, Wewe uwapo karibu.

Nakuhitaji, loo, nakuhitaji!

211 Kama umemchukua Bwana, ipe raha nafsi yake Mbinguni. Tujalie. Tujalie, Bwana.

Mwokozi wangu, naja Kwako!

212 Baba, Mungu, tusikie. Imetupasa kutimiza haki yote hapa. Tunajua vile Neno lisemavyo. Hatumo gizani. Tunajua yale Neno limeahidi. Tusaidie, Ee Bwana, kwamba tutimize haki yote. Litimize Neno Lako. Jalia kila mwaminio hapa awe na imani sasa, tunapokuja kwa wagonjwa. Sisi sote tunapenda kuishi, Bwana; lakini la kwanza ni kuupata Uzima wa Milele, kwa ajili ya ulimwengu huo ujao. Tusikie, Baba, wakati kusanyiko likiomba, hasa sana walio wagonjwa na yeyote anayeteseka.

213 Sijui, yeyote, kama kuna wageni wowote pamoja na sisi, ambao hawajawahi kuwa kwenye maskani hapo awali, nawe ni mgonjwa, na unamtazamia Mungu akusaidie? Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ninyi nyote. Ungeweza kuuinua mkono wako, ninyi watu nisiowafahamu, wasionifahamu mimi ama nisiowafahamu, nanyi mmemjia Kristo sasa mpate usaidizi. Inua tu mkono wako. Unaona? Mungu akubariki, wewe, na wewe. Wapo kadhaa.

214 Inakupasa tu kuamini. Ujumbe huu si wa bure, ni Neno la Mungu.

215 Ninamwona mama fulani...Huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Amebaki ameuinua mkono wake. Ana ugonjwa wa moyo. Yeye ni Bibi Nance. Ametoka Madisonville, Kentucky. Hiyo ni kweli. Sivyoo, mama? Unaweza kuinua kichwa chako

ukitaka. Ulikuwa umeuinua mkono wako, na ukaendelea tu kuuinua. Hiyo ni kweli, sivyo? Kama ni kweli, inua mkono wako. Mnaona mahali tunapoishi, marafiki? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Simjui mama huyo. Sijawahi kumwona. Lakini ni kitu gani? Ni ishara ya Injili. Ili mweze kuninii. . .

216 Unaamini kwamba Mimi ni nabii Wake, mama? Unaamini? Hata hivyo, sisi hatufahamiani. Sikujui. Jina hilo lilikuwa sahihi, sivyo? Kama lilikuwa sahihi, lolote alilokwambia, pu—punga tu mikono yako kwa wasikilizaji, ili waweze kuona kwamba hiyo ilikuwa ni kweli. [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

217 Ni kitu gani kingaliweza kufanya hilo? Yesu wa Nazareti. Mpate kujua ya kwamba mimi ni nabii wa Mungu, na ninawaambia Kweli, kwa kuwa inatupasa. Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Naye akageuka akamwambia, “kutokwa kwake na damu,” akasema kulikuwa kumekwisha.

218 Mama anayeketi karibu na wewe, pia ana ugonjwa wa moyo, pia. Hiyo ni kweli. Naam. Simjui. Unajua sikujui, mama. Lakini Mungu anamjua. Anajua shida yake, sivyo? Bibi Allen, je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? [Huyo mwanamke anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Kama hilo ndilo jina lako na shida yako, inua mkono wako. Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. [Kusanyiko linashangilia.]

219 Mama anayeketi karibu na wewe hapo. Ninamaanisha Bibi Bennett. Nyote mmetoka mahali pamoja. Ana ugonjwa wa figo badala ya ugonjwa wa moyo. Wewe amini kwa moyo wako wote, unaweza kupata afya, pia. Unaamini, mama? Inua mkono wako, na useme, “Nitalikubali,” ndipo unaweza kwenda nyumbani na kupata afya. Kama unaweza kuamini! Nyote mko huko chini Kentucky, mji unaoitwa Madisonville.

220 Mama mmoja, anayeketi moja kwa moja kule nyuma, Bibi Bone. Yeye yuko karibu na Madisonville. Yeye haishi Madisonville kwenyewe, ananiangalia moja kwa moja. Na yule pale Malaika yule amesimama moja kwa moja juu yake. Yeye anaishi tu karibu na Madisonville. Jina lake ni Bone; ugonjwa wa mapindi, ugonjwa wa pumu, kukohoa. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako huku na huku, mama. Mwamini Bwana Yesu Kristo, kisha uende nyumbani ukaponywe.

221 Ugonjwa wa koo, bwana. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuuponya ugonjwa wa koo na kukupa afya? Ponywa! Mwamini Mungu tu.

222 Binti Hopkins, yule binti mweusi kutoka Chikago. Sikujui wewe, sijawahi kukuona maishani mwangu. Lakini unataka kuponywa ugonjwa huo wa neva, ugonjwa wa mapindi? Nenda zako, amini, nawe unaweza kuponywa, pia.

223 Bibi Hanes kutoka Columbus, Ohio. Ukimwamini Bwana Yesu Kristo, unaweza kwenda nyumbani na upate afya, pia.

224 Tumefikia mwisho wa safari. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Inatupasa kutimiza haki yote. Yeye aliahidi mambo hayo yangukwako. Tumewasili. Mnaamini hilo? [“Amina!”]

225 Vema, wekeaneni mikono. Ninataka kuwaulizeni swali. Je! Yesu aliahidi mambo haya yangetokea katika siku za mwisho? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, pia.” Hivi Yeye pia alisema hili, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya?” [“Amina.”] Uko tayari kuchukua msimamo wako, kama mwaminio? [“Amina.”] Kwa kuwa imetupasa kuitimiza haki yote.

226 Ni haki ya Mungu, kwamba wakati lesio hizi hapa (ninaweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu) zitakapowagusa; ninajua Roho Mtakatifu yupo hapa, Yeye yule aliyekuwa pamoja na Paulo. “Walitoa kwa Paulo...” Nanyi mtaponywa, kama mtaamini tu.

227 Ninaamini Roho Mtakatifu yeye yule, kwa Roho Mtakatifu, yupo hapa asubuhi ya leo, akijithibitisha Mwenyewe, Ujumbe wa siku ya mwisho; yule Roho Mtakatifu mkuu Mwenyewe, Mwenyewe akijitwalia mwili, akiingia katika mwili wa kibinadamu, akitenda kazi Zake.

228 Nimesimama asubuhi ya leo, kwa shida. Mnajua karibu kile ninachojiandaa kusikia nitakapoondoka hapa. Lakini imetupasa ya kwamba haki yote itimizwe.

229 Mungu aliweka Ujumbe moyoni mwangu. Sasa inakupasa, kama mwaminio, kwamba uamini. Wakati mkiwa, mmewekeana mikono, hakutakuwako na mgonjwa miongoni mwetu, kama mtaamini hilo tu kwa moyo wenu wote, mwe tayari kuchukua msimamo wenu.

230 Sasa, Baba wa Mbinguni, tunakuletea wasikilizaji hawa, baada ya Ujumbe huu. Bwana Mungu, hakika watu wanaweza kuona sasa ya kwamba inatupasa. Inampasa nabii, kusimama juu ya Neno. Inampasa mfuasi wa kanisa, inawapasa kwamba wasimame. Inawapasa wagonjwa, kuliadini Neno la Yesu Kristo, wakati Yeye aliposema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya.”

231 Nilikuwa nikitaka kufanyiza mstari huo wa maombi, Bwana. Lakini ujumbe ambao umenifikia sasa hivi, kwa simu, umenitikisa, Baba. Ee Mungu, Neno Lako linasema, “Imetupasa kuitimiza haki yote.” Hawa hapa, kila mmoja wao.

232 Roho Mtakatifu yupo hapa akithibitisha kuwa yuko miongoni mwetu. Sasa jalia Nguvu za Mungu, jalia ushuhuda wa Roho Mtakatifu, uingie ndani ya mioyo ya watu hawa sasa hivi, ukiwapa hakikisho; kama vile Danieli alivyokuwa

nalo, kama vile Nuhu alivyokuwa nalo, kama vile Henoko alivyokuwa nalo, kama Yohana alivyokuwa nalo, kama vile Petro alivyokuwa nalo, kama Paulo alivyokuwa nalo, kama vile Yesu alivyokuwa nalo, kama vile Ibrahimu alivyokuwa nalo, kama vile wote walivyokuwa nalo, Bwana. Kwamba, inatupasa sisi katika wakati huu, mahali ambapo nguvu za uponyaji wa Kiungu zimemiminwa, ishara na maajabu yanafanywa, uamsho mkuu umetokea miongoni mwa watu, Roho Mtakatifu ameshuka miongoni mwa watu. Wamepaza sauti, wamenena kwa lugha, wametabiri, karama kuu, na ishara na maajabu. Yule Malaika wa Ujumbe, yule Malaika wa wakati huu ameonekana kwetu katika mfano wa Roho Mtakatifu, Naye anatuletea Ujumbe. Tunauona ukitimizwa. Tunamwona akiichukua miili yetu na kutubadilisha kutoka wanadamu wanaopatikana na mauti, tukawa mawakala wa Mungu, kutangaza ishara kuu na maajabu. Tunapoyaona mambo haya, basi inatupasa kwamba tutimize haki yote.

²³³ Tunapojua ya kwamba Ibrahimu aliangalia nyuma kwa Lutu, kwamba wakati Danieli angeangalia nyuma kwa Ibrahimu, kwamba wakati Yohana angeweza kuangalia nyuma kwa Danieli, (Ee Mungu!) kwamba wakati Petro na Yohana wangeweza kuangalia kwa Yesu. Na wakati tunapoweza kuangalia kwao, na leo hii tunaona matokeo yale yale miongoni mwetu, basi inatupasa kutimiza haki yote.

²³⁴ Nguvu za Yesu na zitapakae kwenye jengo hili, pamoja na imani ya Kiungu, na kumponya kila mtu humu ndani, kila mateso na kila ugonjwa, Bwana. Na, kama mtumishi Wako, ninamwapisha huyu ibilisi ambaye amenisukuma asubuhi yote, ambaye amejaribu kunifanya nitoke humu mimbarani! Kwa neema ya Mungu, nilikaa humu, kwa ajili ya maskini wanadamu hawa wa Mungu walio wagonjwa ama—ama wanaoteseka.

²³⁵ Ondoka ndani yao, Shetani, wewe ibilisi! Ninakuapisha, kwa Yesu Kristo Mungu aliye hai, ya kwamba uwaondokee watu hawa, wala usiwasumbue tena, kwa kuwa wanasimama kama wana wa Kiebrania katika wakati wa majaribu, kuchukua msimamo wao, na waponywe tangu wakati huu na kuendelea. Kupitia Jina la Yesu Kristo, ninayaapisha maradhi na ibilisi wa kusanyiko hili, ambao wamekuja kuwafanya watu hawa kuwa wagonjwa, wawaondokee!

²³⁶ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, mioyo yetu kwa Mungu, nitaimba wimbo. Nitaujaribu, kwa msaada wenu na wa Mungu. *Imani Yangu Inakutegemea Wewe*. Siwatakeni kutilia shaka, hata kidogo, bali ninawatakeni muamini sasa. Inatupasa. Ni Wakristo wangapi walio humu ndani? Inueni mikono yenu, na msemi, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Ni waaminio wangapi? Semeni, “Amina.” [“Amina!”] Ni wangapi mlioweka mikono yenu juu ya wengine? Semeni, “Amina.” [“Amina!”] Basi inatupasa tutimize haki yote.

Imani yangu inakutegemea Wewe,
 Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
 Mwokozi wa kiungu,
 Sasa nisikie ninapoomba,
 Ondolea mbali hatia zangu . . . (Sasa, *dhambi* ni
 “kutokuamini”)
 Ee nijalie tangu leo
 Kuwa Wako kabisa!
 Ninapotembea kwenye mwanambije wa
 maisha,
 Na huzuni zimenizunguka, (Mungu, kuwa
 Kiongozi wangu sasa!)
 Kuwa Kiongozi wangu;
 Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
 Pangusa machozi yote ya huzuni,
 Wala usiniache nikaondoke karibu Nawe.

²³⁷ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Maskini yule mama kipenzi changu ameaga dunia tangu nimekuwa nikihubiri, sauti yangu na irudishe mwangwi kwenye magenge makuu ya Mbinguni.

²³⁸ Wakati yeye aliponiambia, hivi majuzi, alisema, “Billy, umenilisha. Umelipa kodi yangu ya nyumba na bili zangu za umeme, ukanipa chakula.” Kasema, “Mpenzi, ulipokuwa mvulana mdogo, nilitoka kwenye baridi na kukata kuni, nikawasha moto upate kupata joto. Pia nikakupikia chakula, chochote tulichokuwa nacho nyumbani, cha kupika.” Nikimwona amelala pale, na hiyo mikono midogo dhaifu iliyozirosha nguo zetu chafu. Unasimama pale hujiwezi, nisingeweza kufanya lolote.

²³⁹ Nikasema, “Mama, katika mikono ya Mungu aliye hai, ninaiweka nafsi yako yenye haki.”

²⁴⁰ Kama ametuacha tangu wakati huo; wote wametuacha, ndugu zangu ndio tu wamebaki. Ujumbe hapa mimbarani ulikuwa ni mgumu sana. Kama ametuacha, Mungu na aipe raha nafsi yake. Kama angali pamoja nasi, na pamoja nasi hata usiku wa leo, kwa neema ya Mungu nitakuwa hapa mimbarani kutimiza wajibu wangu, kwa kuwa inanipasa niitimize haki yote.

²⁴¹ Wakati nikitafuta kujua, nitamwachia Ndugu Neville ibada, mchungaji mwenzangu mwenye heri.



IMETUPASA KUTIMIZA HAKI YOTE SWA61-1001M

(It Becometh Us To Fulfil All Righteousness)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 1 Oktoba, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha kwa usahihi Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa hadi kwenye ukurasa uliochapishwa, na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsihi hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org